



IA TUJIFUNZE BIBLIA

Kwanza

Kitabu cha Nne



**NZIA ADAMU
MPAKA IBRAHIMU**



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA


Mwaka wa Kwanza

Kitabu cha Nne

Africa Coordinated Curriculum for
Bible Study

Jl - 4P

Published and printed by
Baptist Publications House
Box 30370, , Nairobi



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

Mwaka wa Kwanza

Kitabu cha Nne

Y A L I Y O M O

<u>Sura</u>	<u>Ukurasa</u>
Ujumbe kwa Mwanafunzi.....	4
1. Mungu Aliumba Ulimwengu.....	5
2. Watu Wawili wa Kwanza.....	15
3. Hakuna Mahali pa Kujificha.....	24
4. Ndugu wa Kwanza.....	34
5. Gharika.....	44
6. Upinde Hufuata Gharika.....	54
7. Mungu Asema na Mwanadamu.....	67
8. Amu Asiye na Choyo.....	76
9. Mungu Hushiriki Siri Fulani.....	85
10. Mungu Ashughulika na Wateule Wake.....	95
11. Ahadi Kuu ya Mungu.....	104
12. Kipawa Kikuu Cha Mungu.....	112
13. Mpango Halisi wa Mungu.....	122

UJUMBE KWA MWANAFUNZI

Tazama mahali ulipo. Je! unaona nini? Labda unaona mti, jengo, nyumba, mtu, mbwa, au kitu kingine. Je! vitu hivi vilitoka wapi? Vilifikaje hapo?

Miaka mingi sana iliyopita, ulimwengu haukuwapo. Mungu alikata shauri kuu- mba ulimwengu bila kutumia kitu cho cho- te. Kisha alianza kuumba vitu. Aliumba usiku na mchana, nchi kavu na bahari, miti na wanyama, akamwumba mwanadamu. Tangu mwanzo kila kitu kilikuwa chema. Lakini mwanadamu alijifunza kutenda dha- mbi, na tangu wakati huo ndipo vitu vili- anza kupoteza uzuri wao.

Ulimwengu huu wetu ulianza zamani sana. Vitu vyote tulivyo navyo sasa vili- toka kwa vitu vile vya kwanza ambavyo Mungu wetu aliumba. Hata watu walianza kuwapo wakati Mungu alipoanza kuumba ulimwengu.

Sasa tutajifunza juu ya vitu vya kwanza ambavyo Mungu aliumba, na juu ya jamaa wa kwanza. Tutakuwa na wakati wa kufaraha sana kuona jinsi kazi za Mungu zilivyo za ajabu. Tutaweza kuona jinsi Mungu alivyo na uwezo, na jinsi anavyowe- za kufanya maisha yetu kuwa kama yake.

Mungu aliumba kila kitu kamili kwa matumizi yetu, lakini mwanadamu alikuwa mchoyo. Mwanadamu aliruhusu dhambi kui- ngia maishani mwake. Wakati huu ambapo tunajifunza ahadi za Mungu, hebu tuone ya kwamba alitimiza kila ahadi aliyoa- hidi. Tujifunze ya kwamba sisi pia ni lazima kuwa waaminifu kwa Mungu.

MUNGU ALIUMBA ULIMWENGU


MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo 1:3-38, 2:1-2

Je! unaweza kufikiria jinsi ingekuwa kama hakungekuwapo watu, miti, maua, nuru, na hata ulimwengu? La, ni vigumu sisi kufikiria wakati kama huo. Lakini kulikuwa na wakati ambapo ulimwengu haukuwapo.

Je! unaweza kufikiria jinsi Mungu alivyokuwa peke yake? Hapo mwanzo, Mungu peke yake ndiye aliyekuwapo. Akapanga kuumba viumbe vyote. Alikata shauri kumwumba mwanadamu ili angeweza kusema naye na kuwa na urafiki naye. Kisha angeonyesha upendo wake mkuu kwa mwanadamu.

Kabla Mungu kumwumba mwanadamu, alijua kwamba ilikuwa lazima kumtayarishia (mwanadamu) mahali pa kukaa, kwa hiyo aliumba ulimwengu. Mwanzo 1:3 inasema, "Mungu akasema, Iwe nuru; ikawa nuru." Mungu akatenga nuru na giza, akaita nuru "mchana" na giza akaliita "usiku."

Halafu siku ya pili yake Mungu alisema, "Na liwe anga" (Mwanzo 1:6). Maana ya neno hilo anga ni mbingu kubwa. Alisema anga hilo lingetenga maji yaliyo chini yake na yale yaliyo juu yake. Maji yaliyo juu ya anga ni mawingu. Yale yaliyo chini ya anga ndiyo bahari, maziwa na mito. Lakini siku hii maji yalikuwa yamefunika uso wa nchi.




Siku ya tatu Mungu alifanya mambo mengi kutukia. Aliposema, maji yaliyokuwa yakifunika uso wa nchi yalianza kukusanyika mahali pamoja. Mengine yalikimbia kutoka mlimani na kupitia mabondeni hadi baharini. Maji hayo ndiyo hatimaye yakuwa mito na maziwa na bahari. Katika siku hii pia Mungu alipangia mimea kukua na kutoa mbegu ambazo zingezaa mimea mingine.

Siku ya nne kulikuwa na vitu vingine vitatu ambavyo Mungu aliviumba. Aliumba jua kutoa nuru mchana, na mianga mingine inayotoa nuru usiku. Aliumba mwezi na nyota kutoa nuru usiku.

Siku ya tano ndiyo siku ambayo Mungu aliumba wanyama wa baharini na warukao angani. Je! wanyama wa baharini ni ipi? Ndiyo, ni'samaki. Wanyama wa namna nyingi sana wanakaa baharini. Na ndege wa namna nyingi sana huruka angani.

Kila kitu ambacho Mungu aliumba katika ulimwengu wake kilikuwa kizuri, lakini Mungu hakurudhika. Siku ya sita

MUNGU ALIUMBA ULMWENGU



Mungu aliumba wanyama wanaotembea nchini na wale wanaotambaa. Kisha Mungu akasema, "Na tufanye mtu kwa mfano wetu." (Mwanzo 1:26) Kila kiumbe katika ulimwengu mzuri wa Mungu kilikuwa tayari kwa matumizi ya kiumbe kikuu cha Mungu - mwanadamu. Mungu alimwumba mwanadamu kwa mavumbi ya ardhi. Akampa macho ya kuona, masikio ya kusikia, mdomo wa kula, na miguu ya kutembea. Lakini haya yote hayakutosha kwa sababu Mungu alikuwa amewapa wanyama wengi mau-ngo haya.

Mungu alimpa mwanadamu kitu ambacho hakumpa mnyama ye yote, kitu ambacho kina-mfanya mwanadamu kuwa tofauti kabisa na wanyama wote, na kufanana na Mungu. Mungu anatwambia ya kwamba alimwumba mwanadamu kwa mfano wake. Je! hii maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba Mungu alimpa mwanadamu roho. Alimpa akili, uwezo wa kupenda, na uwezo wa kuchagua jambo ana-lotaka.

Kisha Mungu alisema jambo lingine ambalo lilikuwa la umuhimu sana. Alisema

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

ya kwamba mwanadamu angetawala viumbe vyake vyote alivyoumba. Hii maana yake kwamba, Mungu aliumba vitu vyote ambavyo tumekwisha kutaja ili mwanadamu angeweza kuvifurahia. Mungu alimwumba mwanadamu kuwa rafiki naye na kumpenda. Alitaka mwanadamu kuwa na furaha tele na kupata kitu cho chote ambacho angehitaji. Ili kumfanya mwanadamu kuwa na furaha zaidi Mungu alimwumba mwanamke ili asingeweza kukaa peke yake. Mungu alimwumba Hawa kumsaidia Adamu. Adamu na Hawa ndio waliokuwa mume na mke wa kwanza.

Tunasoma ya kwamba Mungu alimwumba mwanadamu kwa mfano wake. Hii maana yake ni kwamba Mungu alimwumba mwanadamu kufanana naye. Je! unaweza kuona mfano wa Mungu katika maisha yako? Je! unafanana naye katika mambo unayofanya? Mungu alitukusudia kuwa kama yeye na kama hatufanani naye ni kwa sababu tumechagua kuwa wachoyo katika maisha yetu.


Mungu alimaliza kazi yake ya kuumba kwa muda wa siku sita. Siku ya saba Mungu alipumzika, lakini si kwa sababu alichoka, bali ni kwa sababu alimaliza kazi yake. Mungu aliibariki siku hiyo ya saba akaifanya kuwa tofauti na siku nyingine zote. Ni katika siku hii ndipo tunapomwabudu Mungu kama siku iliyotengwa kwa mapumziko. Ni nafasi ya kumsujudia Bwana. Je! sisi huenda kumsujudia Mungu wapi? Ndiyo, sisi huenda kanisani ambapo ni mahali pa ibada. Tunaweza kumwabudu Mungu wakati wo wote na katika mahali po pote, lakini kwa sababu kanisa ndipo mahali pa

MUNGU ALIUMBA ULIMWENGU

ibada, tunapenda kwenda huko kuabudu wakati wo wote ambapo tuna nafasi.

KAZI YA KUFANYA:

Jaza nafasi zilizo katika mchoro unaofuata kuonyesha ni siku ipi ambayo Mungu aliumba kitu hicho ambacho kimechorwa. Pia, andika namba ya kifungu cha Biblia kutoka Mwanzo 1 au 2 kinachotusimulia kuhusu kazi ya siku ile.



Jaza nafasi zifuatazo:

Siku ya Kwanza: Siku ya kwanza Mungu alisema, kuwaka _____.


Siku ya Pili: Siku ya pili Mungu alisema, "Na liwe anga." Maana yake mbingu. Taja baadhi ya maji yaliyo chini ya anga. _____, na _____.

Siku ya Tatu: Siku ya tatu maji yali-kuwa bado yamefunika uso wote wa nchi. Sasa Mungu aliyatenga maji hayo na nchi. Je! aliyafanya nini kukua katika nchi kavu? _____, _____, na _____.


Siku ya Nne: Je! ni mianga ipi ambayo Mungu aliumba kutoa nuru wakati wa mchana na wakati wa usiku? _____, na _____.

Siku ya Tano: Siku ya tano Mungu aliumba kitu kirukacho angani na kingine kinachoogelea baharini. Chora picha ya vitu hivyo ambavyo Mungu aliumba siku ya tano.

MUNGU ALIUMBA ULMWENGU



Ninaruka
angani.



Ninaogelea
baharini.

Siku ya Sita: Kata majina yote ya
vitu ambavyo Mungu
hakuumba siku ya sita.

MITI
WANAWAKE

NDEGE
MAJANI

NG'OMBE
MAUA

WATU
MITO

SAMAKI
MAWINGO

Siku ya Saba: Je! Mungu alifanya
nini siku ya saba?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

*"Njoni, tuabudu, tusujudu, tupige
magoti mbele za Bwana aliyetuumba.
Kwa maana ndiye Mungu wetu."*

Zaburi 95:6-7

Fikiria mtu mkuu aliyeumba vitu
vyote; ulimwengu, viumbe, na wewe. Kifu-
ngu chako cha kukumbuka kingeeleza jinsi
ungemfikiria Mwumba wako. Kuabudu maana
yake ni kumheshimu Mungu. Andika maombi
ya ibada kwa Mwumba wako katika mistari
hiyo hapo chini.

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

MANENO YA KUJIFUNZA:

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Mwanzo 1:3-28

Mungu akasema, Iwe nuru; ikawa nuru. (4) Mungu akaiona nuru, ya-kuwa ni njema; Mungu akatenga nuru na giza. (5) Mungu akaliita nuru Mchana, na giza akaliita Usiku. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku moja.

(6) Mungu akasema, Na liwe anga kati-kati ya maji, likayatenge maji na maji.

(7) Mungu akalifanya anga, akayatenga yale maji yaliyo juu ya anga na yale maji yaliyo chini ya anga; ikawa hivyo. (8) Mungu akaliita lile anga Mbingu. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya pili.

(9) Mungu akasema, Maji yaliyo chini ya mbingu na yakusanyike mahali pamoja, ili pakavu paonekane; ikawa hivyo. (10) Mungu akapaita pale pakavu Nchi; na maku-sanyiko ya maji akayaita Bahari; Mungu akaona ya kuwa ni vyema. (11) Mungu akasema, Nchi na itoe majani, mche utoao mbegu, na mti wa matunda uzao matunda kwa jinsi yake, ambao mbegu zake zimo ndani yake, juu ya nchi; ikawa hivyo. (12) Nchi ikatoa majani, mche utoao mbegu kwa jinsi yake, na mti uzao matunda, ambao mbegu zake zimo ndani yake, kwa

jinsi yake, na mti uzaao matunda, ambao mbegu zake zimo ndani yake, kwa jinsi yake; Mungu akaona ya kuwa ni vyema.

(13) Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya tatu.

(14) Mungu akasema, Na iwe mianga katika anga la mbingu ili itenge kati ya mchana na usiku; nayo iwe ndiyo dalili

na majira na siku na miaka; (15) tena iwe ndiyo mianga katika anga la mbingu itie nuru juu ya nchi; ikawa hivyo. (16)

Mungu akafanya mianga miwili mikubwa, ule mkubwa utawale mchana, na ule mdogo utawale usiku; akafanya na nyota pia.

(17) Mungu akaiweka katika anga la mbingu, itie nuru juu ya nchi (18) na kuutawala mchana na usiku na kutenga nuru na giza; Mungu akaona ya kuwa ni vyema. (19) Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya nne.

(20) Mungu akasema, Maji na yajawe kwa wingi na kitu kiendacho chenye uhai, na ndege waruke juu ya nchi katika anga la mbingu. (21) Mungu akaumba nyangumi wakubwa, na kila kiumbe chenye uhai kie-ndacho, ambavyo maji yalijava navyo kwa wingi kwa jinsi zao, na kila ndege aruka-ye, kwa jinsi yake; Mungu akaona ya kuwa ni vyema. (22) Mungu akavibarikia, akise-
ma, Zaeni, mkaongezeke, mkayajaze maji ya baharini, ndege na wazidi katika nchi. (23) Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya tano.

(24) Mungu akasema, Nchi na izaie kiumbe hai kwa jinsi zake, mnyama wa kufu-
gwa, nacho kitambaacho, na wanyama wa mwitu kwa jinsi zake; ikawa hivyo. (25) Mungu akafanya mnyama wa mwitu kwa jinsi zake, na mnyama wa kufugwa kwa jinsi zake,

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

na kila kitu kitambaacho juu ya nchi kwa jinsi yake; Mungu akaona ya kuwa ni vyema. (26) Mungu akasema, Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. (27) Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwana-mume na mwanamke aliwaumba. (28) Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kienda-cho juu ya nchi.

Mwanzo 2:1-2

Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote. (2) Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya.

WATU WAWILI WA KWANZA

MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo 2:5-9; 15-23

Kila wakati ambapo Mungu aliumba kitu kipya kwa ulimwengu wake, alisema tu, kwa mfano "Iwe nuru," au "Pakavu paonekane," au alitoa amri fulani. Kama alivyosema ndivyo iliyofanyika. Sasa, wakati maalum ulikuwa umefika ambao kwa ajili yake aliutayarisha ulimwengu. Wakati huu Mungu alifanya kazi yake kati-ka njia tofauti. Alitumia vifaa vya ardhi kumwumba mtu wa kwanza. Alimwumba mtu kwa mavumbi ya ardhi. Kisha akampulizia puani pumzi ya uhai. Kwa njia hii, Mungu alimfanya mwanadamu kuwa nafsi iliyo hai.

Mungu alimwumba mtu wa kwanza kwa mfano wake. Hii si kusema kwamba mwili wa Adamu ulikuwa kama wa Mungu kwa sababu Mungu hana mwili kama wa mwanadamu. Adamu alifanana na Mungu kwa kuweza kufikiri na kukata shauri yeye mwenyewe juu ya jambo la kufanya. Alifanana na Mungu kwa sababu alikuwa na upendo tena alitaka kupendwa. Alifanana sana na Mungu hata Mungu akamchagua kuwa rafiki yake.



Mungu alimpa rafiki yake huyu mpya makao. Makao hayo yalikuwa mazuri sana katika mahali palipoitwa Bustani ya Edeni. Mungu mwenyewe ndiye aliyepanda bustani hiyo. Vitu vyote ambavyo

Mungu aliumba, kwa mfano nchi, viumbe vyote vinavyoishi, maua na miti, vyote vilikuwa vya mwanadamu kwa sababu Mungu aliyeviumba alivitoa kwa mwanadamu. Alimwambia mwanadamu kuvipa majina na kuvitunza na kuvifurahia vyote.

Mungu alimpangia mwanadamu kutumia akili na mwili wake. Alimpa kazi ya kufanya. Kazi aliyompa mwanadamu kufanya katika Bustani ya Edeni ilikuwa ni kuilima na kuitunza. Hatujui mambo yote ambayo yalimbidi Adamu kufanya, lakini Mwanzo 2:15 inatuonyesha kwamba Adamu alipewa kazi ya kufanya.

Mungu alitaka Adamu kuwa na furaha nyingi. Hakutaka Adamu kuwa na huzuni au kuwa peke yake. Kwa hiyo Mungu alimwumba mtu mwingine, yaani, mwanamke wa kwanza. Badala ya kumwumba mwanamke kwa mavumbi ya ardhi kama alivyomwumba mwanamume, Mungu alimwumba Hawa kwa sehemu ya maungo ya Adamu. Mungu alimletea Adamu usingizi mzito, akalala. Kisha Mungu akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake. Kwa ubavu ule aliotwaa kwa Adamu, Mungu alimwumba mwanamke. Mwanamke angekuwa msaidizi wa Adamu na angekaa naye. Basi katika Bustani ya Edeni, mwanamume wa kwanza (Adamu) na mwanamke wa kwanza (Hawa) ndio waliokuwa jamaa wa kwanza. Walikuwa huru kufurahia na kutumia vitu vyote ambavyo Mungu aliumba.

Mungu alimpa Adamu amri moja. Kulikuwa na miti miwili katika bustani ile ambayo ilikuwa na majina tofauti na ya miti tuliyo nayo sasa. Je! unajua majina

yao? Miti hiyo miwili iliitwa Mti 'wa Uzima, na Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya. Mungu alimwambia Adamu kwamba angeweza kula matunda ya kila mti mle bustanini isipokuwa ya mti mmoja. Alimwambia Adamu ya kwamba angekufa kama angekula tunda la Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya. Alimtumainia Adamu kumtii. Adamu alikuwa na nafasi ya kumwonyesha Mungu kwamba alimpenda na kwamba angemtii. Mungu alikuwa amempa vitu vingi. Sasa ilikuwa nafasi ya Adamu kumtii Mungu. Hili tu ndilo jambo ambalo Mungu alimtaka Adamu kumfanyia.

Jambo hili lilipotimizwa, Mungu alikuwa sasa amemaliza kazi yake ya kuumba. Alifurahia sana ulimwengu wake mpya, wanyama wapya, miti mipya, mwezi mpya na nyota mpya. Mungu alifurahia hasa kiumbe chake kipya, mwanadamu. Alipotazama kazi hii yake, alisema ni njema sana.

Wakati Mungu alipomaliza kazi yake, alipanga wakati wa kupumzika. Alipumzika siku ya saba akaiita siku hiyo kuwa ni siku maalum. Mwanzo 2:3 inasema kwamba Mungu aliibariki siku ya saba akaitakasa. Yatupasa kumwabudu Muumba wetu. Tunataka kumwonyesha kwamba tunampenda na kwamba tunataka kumtii. Ni kwa jinsi gani tunaweza kumwabudu Mungu leo? Tunaweza kumwabudu kwa kuomba kwa heshima, kwa kusikiliza masomo ya Biblia, na kwa kumtii mwalimu au mhubiri wetu. Tunaweza kumwabudu Mungu kwa kutoa sadaka zetu kwa Bwana. Tunaweza kumwabudu kwa kuwasaidia wengine. Zaidi ya yote, tunaweza kumwabudu Mungu kwa kumpenda na kwa kutaka kumtii kila siku.

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

KAZI YA KUFANYA:

Soma zaidi juu ya ulimwengu mpya wa Mungu wa ajabu, na mtu ambaye Mungu aliumba katika Mwanzo 2:5-8. Kisha chora mviringo kwa jibu sawa la kila swali.

Ulimwengu ulitiwaje maji?

Mvua ilinyesha

Ukungu ulipanda
katika nchi

Mungu Bwana alimwumba mwanadamu kwa kutumia nini?

Mavumbi ya
ardhi

Matawi ya mti

Ni nani aliyempulizia mwanadamu pumzi ya uhai?

Adamu

Mungu

Mungu alifanya nini kuwa makao ya mwanadamu?

Nyumba ndogo
ya majani

Bustani ya Edeni

Jaza nafasi zilizoachwa katika sentensi zifuatazo:

Je! miti ile miwili katika Bustani ya Edeni iliitwaje?

Mti wa _____.

Mti wa _____ wa _____
na _____.

WATU WAWILI WA KWANZA

Je! Mungu alimpa Adamu kazi gani ya kufanya?

Je! unafikiri Adamu alifurahia kazi hii? _____ kwa nini?

Bwana alimpenda Adamu sana. Alimpa kila kitu ambacho alihitaji kwa furaha yake. Pia alimpa nafasi ya kuthibitisha kwamba alimpenda Bwana yake, kwa sababu alimpa sheria kuitii. Jifanye kuwa Adamu. Andika maneno ambayo Mungu anakwambia kufanya na yale ambayo hupaswi kufanya. Unaweza kupata majibu haya katika Mwanzo 2:16-17.

Naweza _____

_____.


Siwezi _____

_____.

Je! Mungu alimpa Adamu amri ngapi?

_____.

Tazama picha hapo chini. Andika orodha ya vitu vyote ambavyo Mungu aliweka katika Bustani ya Edeni kwa ajili ya Adamu kuvifurahia.



Je! ni kwa nini Mungu alimwambia Adamu msaidizi?

Kwa sababu haikuwa _____ kwa Adamu kuwa _____.

Je! Mungu alimfanyia Adamu kufanya nini?

Je! Mungu alitwaa nini kutoka kwa Adamu? _____

Je! kwa kitu hicho Mungu alichokitoe kutoka kwa Adamu aliumba nini?

WATU WAWILI WA KWANZA

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

*"Nimeichagua njia ya uaminifu, na
kuziweka hukumu zako mbele yangu."
Zaburi 119:30*

Wakati Mungu alipomwumba Adamu ali-
mpa uwezo wa kuchagua kati ya mema na
mabaya. Adamu angechagua kutii au kutotii
amri ya Mungu. Wewe pia una uwezo huu wa
kuchagua. Ukichagua kuamini na kumtii
Mungu, atajaza maisha yako na mambo mema.
Piga mstari chini ya vitu ambavyo Mungu
atakupa kama ukichagua kumtii.

Nguvu katika majaribu
Marafiki Wakristo
Upendo kwa Wengine
Msaada katika wakati wa taabu
Upendo kwa Neno la Mungu

MANENO YA KUJIFUNZA:

maungu.....vitu vinavyofunganisha
vitu pamoja, sehemu
zo zote za mwili

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Mwanzo 2:5-9

Hapakuwa na mche wa kondeni bado,
wala mboga ya kondeni haijachipuka bado,
kwa maana BWANA Mungu hajainyeshea nchi
mvua, wala hapana mtu wa kuilima ardhi;
(6) ukungu ukapanda katika nchi, ukatia
maji juu ya uso wote wa ardhi. (7) BWANA

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai. (8) BWANA Mungu akapanda bustani upande wa mashariki wa Edeni, akamweka ndani yake huyo mtu aliyemfanya. (9) BWANA Mungu akachipusha katika ardhi kila mti unaotamanika kwa macho na kufaa kwa kuliwa; na mti wa uzima katikati ya bustani, na mti wa ujuzi wa wema na mabaya.

Mwanzo 2:15-23

BWANA Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza. (16) BWANA Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, (17) walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.

(18) BWANA Mungu akasema, Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye. (19) BWANA Mungu akafanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa msituni, na kila ndege wa angani, akamletea Adamu ili aone atawaitaje; kila kiumbe hai, jina alilokiita Adamu likawa ndilo jina lake. (20) Adamu akawa pa majina yao kila mnyama wa kufugwa, na ndege wa angani, na kila mnyama wa mwituni; lakini hakuonekana wa kumsaidia Adamu aliyefanana naye. (21) BWANA Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake, (22) na ule ubavu aliotwaa katika Adamu BWANA Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu. (23) Adamu

WATU WAWILI WA KWANZA

akasema, Sasa huyu ni mfupa katika mifupa
yangu, na nyama katika nyama yangu, basi
ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa
katika mwanamume.

HAKUNA MAHALI PA KUJIFICHA

MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo 3:1-24

Siku moja wakati mkewe Adamu alipo-kuwa peke yake alimsikia mtu mmoja akisema. Mtu huyo hakuwa Mungu wala mumewe. Alikuwa mmojawapo wa wanyama! Je! alikuwa mnyama yupi? Ndiyo, alikuwa nyoka. Lakini si nyoka hasa ndiye aliyesema na Hawa. Ni Shetani ndiye alichukua umbo la nyoka na kusema naye. Shetani ni roho. Hana mwili. Basi wakati Shetani alipotaka kusema na mkewe Adamu, alitumia umbo la nyoka ambaye kwa wakati ule alikuwa mnyama mwerevu kuliko wanyama wote ambao Mungu aliumba.

Shetani alimwambia Hawa, "Ati! hivi ndivyo alivyosema Mungu, "Msile matunda ya miti yote ya bustani?" (Mwanzo 3:1) Je! ni kwa nini Shetani alimtaka Hawa kufikiri kwamba Mungu hakuwa mwema kwa kuwakataza kula tunda la mti mmoja? Shetani alijua mambo yale ambayo Mungu aliwaambia Adamu na Hawa msaidizi wake. Hawa alimjibu Shetani ya kwamba Mungu aliwakataza kugusa wala kula tunda la mti ule aliowakataza.

Kisha Shetani alimwambia Hawa uwongo. Alisema, "Hakika hamtakufa. " (Mwanzo 3:4) Lakini Mungu aliwaambia ya kwamba wangekufa. Shetani alimwambia Hawa ya kwamba Mungu hakutaka waonje tunda la mti ule kwa sababu wangepewa kuwa kama Mungu. Shetani alisema ati kama wangepata tunda la mti ule wangepewa kama Mungu kwa

HAKUNA MAHALI PA KUJIFICHA

— Hawa aliona ya kuwa tunda lile lilifaa kwa kula, na lilipendeza macho, na kwamba lingempa ujuzi.

— Walijificha kati ya miti ya bustani.

— Adamu na mkewe sasa walijijua kuwa wa uchi, kwa hiyo walisho-na majani ya mtini, wakajifanyia nguo.

— Hawa alitwaa tunda, akala.

Ona jinsi Adamu na Hawa walivyotoa udhuru kwa Mungu.

Je! Adamu alimlaumu nani kwa kutotii kwake? _____

Je! Hawa alimlaumu nani kwa dhambi yake? _____

Jaza nafasi zifuatazo kuonyesha mabadiliko ambayo dhambi ilileta ulimwengu.

**KABLA YA ADAMU
KUTENDA DHAMBI**

1. Ni mimea _____
peke yake ndiyo
iliyokua katika
ardhi.

**BAADA YA ADAMU
KUTENDA DHAMBI**

1. _____ na _____
ilikua pamoja na
mimea mizuri.

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

KABLA YA ADAMU KUTENDA DHAMBI

BAADA YA ADAMU KUTENDA DHAMBI

2. Nyoka pengine
ndiye aliye-
kuwa mnyama
_____ kuliko
wanyama wote
wa mwitu.

2. Nyoka _____
badala ya kute-
mbea.

3. Mungu _____
Adamu chakula
chake chote

3. Ilimbidi Adamu
_____ kwa
bidii ndipo apate
chakula chake.


Mungu alikusudia kuwaadhibu Adamu na mkewe kwa sababu yeye ni Mtakatifu. Laki- ni alikuwa bado anawapenda ingawa waliko- sa kumtii. Chora mstari kutoka kwa kila swali hadi kwa picha ambayo ni jibu lake.



Mungu hakumtaka Adamu kupata chakula chake kutoka wapi?



Ni nani aliyejifunza tofauti kati ya mema na mabaya?



Adamu na mkewe walifuku- zwa kutoka wapi?



Ni nani ambaye Mungu alimweka upande wa masha- riki ya bustani kulinda mti wa uzima?



mi- wa ujuzi
wa mema na
mabaya

Ni kitu kipi kingine ambacho Mungu alitumia kuwazuia Adamu na Hawa kufikia mti ule wa uzima?

HAKUNA MAHALI PA KUJIFICHA

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

*"Macho ya Bwana yako kila mahali,
yakimchunguza mbaya na mwema."
Mithali 15:3*

Je! Adamu na Hawa wangeweza kujifi-
cha kutoka machoni pa Mungu? _____.
Je! tunaweza kuficha dhambi zetu ili
Mungu asijue? _____.

MANENO YA KUJIFUNZA:

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Mwanzo 3:1-24

Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya BWANA Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani? (2) Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustani twaweza kula; (3) lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa. (4) Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa, (5) kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya. (6) Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi

alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala. (7) Wakafumbuliwa macho wote wawili wakajijua kuwa wa uchi, wakashona majani ya mtini, wakajifanyia nguo. (8) Kisha wakasikia sauti ya BWANA Mungu, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga; Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, BWANA Mungu asiwaone. (9) BWANA Mungu akamwita Adamu, akamwambia, Uko wapi? (10) Akasema, Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha. (11) Akasema, Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale? (12) Adamu akasema, Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala. (13) BWANA Mungu akamwambia mwanamke, Nini hili ulilolifanya? Mwanamke akasema, Nyoka alinidanganya, nikala. (14) BWANA Mungu akamwambia nyoka, Kwa sababu umeyafanya hayo, umelaaniwa wewe kuliko wanyama wote, na kuliko hayawani wote walioko mwituni; kwa tumbo utakwenda, na mavumbi utakula siku zote za maisha yako; (15) nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino. (16) Akamwambia mwanamke, Hakika nitakuzidisha uchungu wako, na kuzaa kwako; kwa utungu utazaa watoto; na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala. (17) Akamwambia Adamu, Kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza, nikisema, Usiyale; ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za

maisha yako; (18) michongona na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za konde-ni; (19) kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavu-mbi wewe, nawe mavumbini utarudi.

(20) Adamu akamwita mkewe jina lake Hawa; kwa kuwa yeye ndiye aliye mama yao wote walio hai. (21) BWANA Mungu akawafanyia Adamu na mkewe mavazi ya ngozi, akawavika.

(22) BWANA Mungu akasema, Basi, huyu mtu amekuwa kama mmoja wetu, kwa kujua mema na mabaya; na sasa asiye akanyosha mkono wake akatwaa matunda ya mti wa uzima, akala, akaishi milele; (23) kwa hiyo BWANA Mungu akamtoa katika bustani ya Edeni, ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa. (24) Basi akamfukuza huyo mtu, akaweka Makerubi, upande wa mashariki wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kuilinda njia ya mti wa uzima.

NDUGU WA KWANZA

MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo 4:1-16

Baada ya muda mfupi, Adamu (mwana-mume wa kwanza) na Hawa (mwanamke wa kwanza) walipata mtoto mume. Kisha katika wakati unaofaa wakapata mtoto mwingine mume. Bila shaka Adamu na Hawa waliwafundisha vijana hawa wao habari za Mungu na jinsi ya kumwabudu. Bila shaka waliwasimulia Kaini na Habili jinsi walivyote-nda dhambi na kutoweza tena kusema na Mungu kama walivyofanya wakati walipoku-wa bustanini. Vijana hawa pia hawangeweza kusema na Mungu waziwazi kama vile wangelipenda, na Mungu pia hangeweza kusema nao waziwazi. Walikuwa na njia ya dhambi ya wazazi wao. Bila shaka walihuzunika kwa ajili ya dhambi kuingia maishani mwao.

Mungu aliwafundisha jambo fulani ambalo lingewapasa kufanya kama wangetaka kumwendea. Lakini hatujui hasa jambo hilo ambalo Mungu aliwaambia kufanya kwa saba-bu halikuandikwa katika kitabu chake, walakini inadhaniwa kwamba aliwaambia kumchinja mnyama fulani, pengine mwana-kondoo na kumtolea kama sadaka ya kuteke-tezwa kuonyesha huzuni yao juu ya dhambi zao.

Baadaye Mungu aliwapa watu wake maongozi jinsi ya kuwatoa wanyama sadaka ya kuteketezwa kwa ajili ya dhambi zao. Wanyama hao hawakuwa na hatia wala hawakustahili kufa, lakini walikufa badala,

ya mtu mwenye dhambi. Mungu alipokea sadaka kama hizo na kusamehe dhambi za wale waliozitoa. Mnyama alikuwa mfano wa Mwana wa Mungu ambaye angekuja ulimwenguni na kufa msalabani ili kuondoa dhambi zao. Hatutoi sadaka za wanyama siku hizi kwa sababu Kristo alikwisha kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Mungu apokea sadaka ya Kristo ya damu yake yenye thamani sana kama sadaka halisi ya dhambi zetu. Tunapokea sadaka ya Kristo kwa imani, Mungu naye hutupokea.

Katika kukua kwao, Kaini na Habili walijifunza jinsi ya kufanya kazi. Habili alikuwa mchungaji. Alichunga kondoo za baba yake. Lakini Kaini alipendelea ukulima. Akiwa kama mkulima, Kaini alipanda mbegu, alitoa kwekwe, na alivuna mavuno yake.

Siku moja, Kaini na Habili walileta sadaka zao kwa Bwana, pengine kama wali-vyomwona baba yao akifanya. Kwa vile Kaini alikuwa mkulima na Habili mchungaji, Kaini alileta mazao ya ardhi na Habili akaleta kondoo aliyofuga. Tunafikiri ya kwamba sadaka hizo zote zilikuwa nzuri, lakini Bwana hakufikiri hivyo. Mungu alipendezwa na sadaka ya Habili na hakupendezwa na ya Kaini. Mungu amekwisha kutwambia ya kwamba Habili alitoa "Sadaka nzuri kuliko Kaini" kwa sababu aliileta kwa imani. Hii maana yake ni kwamba Habili alimwamini Mungu na kumtii kwa kumletea namna ya sadaka aliyotaka.

Walakini, Kaini hakumwamini Mungu. Hakudhani ya kwamba Mungu alitaka sadaka kama alivyosema. Mungu alimwonyesha Kaini ya kwamba hakupendezwa na sadaka yake. Lakini hakupendezwa nayo kwa sababu kondoo wa Habili alikuwa na thamani nyingi kuliko mazao yake. Labda shamba la Kaini lilizaa mazao mengi mema zaidi kuliko kondoo wa Habili. Mungu alipendezwa na sadaka ya Habili kwa sababu Habili alimwamini na kumtii. Alimjia Mungu kama Mungu alivyoagiza. Lakini Kaini hakumwamini Mungu wala kumtii.

Kaini alipoona kwamba Mungu hakupokea sadaka yake, alikasirika sana. Ingawa alimkasirikia Mungu, hakuonyesha dalili ya kusikitika kwa ajili ya kutomtii Mungu. Mungu alisema naye, akampa nafasi nyingine apate kutubu. Lakini Kaini alikuwa mkaidi. Hakumtii Mungu. Tunaweza kuona jinsi dhambi ilivyokuwa ikikua moyoni mwa Kaini. Kwanza, hakumwamini Mungu. Hakumtii. Pili, alimtenda Mungu dhambi kwa kukasirika.

Lakini Kaini hakumkasirikia Mungu peke yake. Wakati Mungu alipoikataa sadaka yake na kupokea sadaka ya Habili nduguye, Kaini alimkasirikia Habili na kumwonea wivu. Chuki mbaya ilijaza moyo wake.

Hata siku moja, Kaini na Habili walikuwa peke yao uwandani. Kaini alimwua Habili nduguye. Shetani alimshawishi Kaini kutenda jambo hili la uovu kama alivyowashawishi wazazi wao kutenda dhambi. Kaini alijifunza ya kwamba mtu

anapokubali majaribu ya Shetani na kute-nda dhambi ya kwanza, dhambi hiyo ita-mwongoza kutenda dhambi nyingine. Sasa ilikuwa rahisi kwa Shetani kumfanya Kaini kutenda mambo maovu. Yeye Kaini ambaye alikuwa kijana wa kwanza kuzaliwa ulimwenguni, alikua, akawa mwuaji wa kwanza.

Mtu fulani alimwona Kaini akimwua nduguye ambaye hakuwa na hatia. Mtu huyo ni yule aliyewaona Adamu na Hawa wakati walipokula tunda la mti waliokatazwa katika Bustani ya Edeni. Je! mtu huyo alikuwa nani? Ndiyo, alikuwa Mungu. Kaini alitambua kwamba hangeweza kujificha kutoka machoni pa Mungu.

Mungu alimwuliza Kaini kwamba nduguye alikuwa wapi. Badala ya kusema ukweli, Kaini alimjibu Mungu, akisema, "Sijui, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?"

Lakini Mungu alijua mahali ambapo Habili nduguye Kaini alikuwa, na alimfanya Kaini kufahamu kwamba alijua habari yake. Alimwambia Kaini ya kwamba sauti ya damu ya nduguye ilikuwa ikiimlilia kuto-ka katika ardhi. Kaini aliogopa sana. Ndipo alijua kwamba Mungu aliona hatia yake na kujua mambo yote. Pia, Mungu alijua kwamba Kaini alisema uwongo tena. Dhambi ilikuwa ikiendelea kuongezeka maishani mwa Kaini.

Kaini alijua wazi ya kwamba Mungu aliadhibu dhambi. Alikuwa na wasiwasi mwingi juu ya adhabu yake kuliko vile juu ya dhambi yake.

Mungu alimwadhibu Kaini katika njia mbili. Kwanza, Kaini alizoea kupanda mbegu na mbegu hizo ziliota na kuwa mimea ambayo ilimzalia yeye na jamaa yake chakula. Sasa ingekuwa vigumu sana kwake kupata chakula kwa sababu ardhi haingempatia mazao. Pili, Mungu alimwambia Kaini ya kwamba angekuwa mtoro asiye na kikao. Hangeweza kukaa mahali pamoja kulima na kuwa na nyumba yake. Daima angehama-hama hapa na pale.

Kaini aliposikia jinsi adhabu yake ingekuwa, alihuzunika sana. Alisema, "Adhabu yangu imenikulia kubwa, haichukuliki." (Mwanzo 4:13) Mpaka sasa Kaini hakuhuzunika kwa ajili ya dhambi yake. Hakumwomba Bwana kumsamehe. Alihuzunika tu ya kwamba dhambi yake ilijulikana. Alikuwa akijifikiria tu yeye mwenyewe. Alikuwa mchoyo. Hii ni dhambi nyingine tena ambayo Kaini alifanya. Kaini aliogopa ya kwamba ye yote ambaye angemwona angejaribu kumwua. "Bwana akamtia Kaini alama mtu amwonaye asiye akampiga." (Mwanzo 4:15) Kaini alitoka katika nchi yake na kuwaacha jamaa yake, akaenda kukaa katika nchi ya Nodi. Aliteseka sana kwa ajili ya dhambi yake kwa sababu alimsikiliza Shetani badala ya kumsikiliza Mungu. Dhambi yake ilimtenga na Mungu.

KAZI YA KUFANYA:

Andika jina la mtoto wa kwanza
Adamu na Hawa. _____

Andika jina la mtoto wao wa pili.

Picha hizo hapo chini zinaonyesha mambo ambayo vijana hawa walifanya wakati wa kukua kwao. Andika jina la kila kijana kando ya picha yake.



Siku moja ndugu hawa wawili walileta sadaka zao kwa Mungu. Chora mviringo kwa sadaka iliyompendeza Mungu.



Sadaka ya Habil
kwa Mungu

Sadaka ya Kaini
kwa Mungu

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

Jaza nafasi zifuatazo kwa majina ya watu wanaoelezwa habari zao.

_____ Aliuawa na nduguye uwandani.

_____ Aliuliza, "Yuko wapi Habili, ndugu yako?"

_____ Alidanganya kwa kusema, "Sijui."

_____ Alimjibu, akasema, "Sauti ya damu ya ndugu yako inanililia kutoka katika ardhi."

Andika orodha ya dhambi ambazo Kaini alifanya.

Mungu huadhibu dhambi. Alimwambia Kaini ya kwamba ilikuwa lazima kufanya kazi shambani mwake kupanda mimea, na kwamba mimea ingemzalia mazao machache sana kwa sababu ya dhambi yake. Pia Mungu alisema ya kwamba Kaini hangeweza kukaa mahali pamoja. Ni maneno gani katika kifungu cha 12 yanayoonyesha kwamba Kaini ni lazima kuhama-hama?

Andika herufi "K" kando ya sentensi iliyo kweli, na uandike herufi "M" kando ya sentensi ambayo si kweli.

— Kaini alihuzunika sana ya kwamba alitenda dhambi.

— Kaini alihuzunika sana ya kwamba angeadhibiwa na Mungu.

— Kaini aliogopa kwamba watu wange-mwua.

— Mungu alimtia Kaini alama ili watu wangemjua na kutojaribu kumwua.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Damu yake Yesu, Mwana wake, yatusa-fisha dhambi yote." I Yohana 1:7

Je! umefanya dhambi? Mungu asema ya kwamba watu wote ambao hawajasamehewa dhambi zao wataadhibiwa. Pia Mungu asema kwamba damu ni lazima kumwagwa ili dhambi ziweze kusamehewa. Katika siku za Agano la Kale, wenye dhambi waliotaka kuishi haki mbele za Mungu walitoa sadaka za wanyama. Njia ya pekee ya kumwendea Mungu ni kwa damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, aliyemwaga damu yake msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. Wale wanaomwamini wamekwisha kusamehewa dhambi zao. Je! unamwamini Yesu kama Mwokozi wako anayekuokoa katika dhambi? _____

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

MANENO YA KUJIFUNZA:

uwanda.....nchi iliyo sawasawa
bila vilima, tambarare
mtoro.....mtu atorokaye, aachaye
kazi bila ruhusa

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Mwanzo 4:1-16

Adamu akamjua Hawa mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Kaini, akasema, Nimepata mtoto mwanamume kwa BWANA. (2) Akamongeza akamzaa ndugu yake, Habilu. Habilu alikuwa mchungu kondoo, na Kaini alikuwa mkulima ardhi. (3) Ikawa hatimaye Kaini akaleta mazao ya ardhi, sadaka kwa BWANA. (4) Habilu naye akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama. BWANA akamtakabali Habilu na sadaka yake; (5) bali Kaini hakumtakabali, wala sadaka yake. Kaini akaghadhibika sana, uso wake ukakunjamana. (6) BWANA akamwambia Kaini, Kwa nini una gadhabu? na kwa nini uso wako umekunjamana? (7) Kama ukitenda vyema, hutapata kibali? Usipotenda vyema dhambi iko, inakuotea mlangoni, nayo inakutamani wewe, walakini yapasa uishinde.

(8) Kaini akamwambia Habilu nduguye, (Tende uwandani). Ikawa walipokuwapo uwandani, Kaini akamwinukia Habilu nduguye, akamwua. (9) BWANA akamwambia Kaini, Yuko wapi Habilu ndugu yako? Akasema, Sijui, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu? (10) Akasema, Umefanya nini? Sauti ya damu ya ndugu yako inanililia kutoka katika ardhi. (11) Basi sasa, umelaaniwa

wewe katika ardhi, iliyofumbua kinywa chake ipokee damu ya ndugu yako kwa mkono wako; (12) utakapoilima ardhi haitakupa mazao yake; utakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani. (13) Kaini akamwambia BWANA, Adhabu yangu imenikulia kubwa, haichukuliki. (14) Tazama, umenifukuza leo katika uso wa ardhi, nitasitirika mbali na uso wako, nami nitakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani; hata itakuwa kila anionaye ataniua. (15) BWANA akamwambia Kwa sababu hiyo ye yote atakayemwua Kaini atalipizwa kisasi mara saba. BWANA akamtia Kaini alama, mtu amwonaye asiye akampiga.

(16) Kaini akatoka mbele za uso wa BWANA, akakaa katika nchi ya Nodi, mbele ya Edeni.

GHARIKA

MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo 6:5-7:5

Baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, bila shaka waliwaonya watoto wao juu ya huzuni inayoletwa na dhambi. Lakini Kaini alitenda dhambi mbaya mno.

Je! baada ya dhambi za Kaini, watu walijifunza juu ya mambo mabaya mno ambayo yanguwajia kama wangekaa katika dhambi? La. Watu waliendelea tu kujaribu kuishi katika njia ambayo iliwapendeza wao wenyewe na kutojali kumpendeza Mungu. Walitenda mambo kana kwamba dhambi haingewadhuru. Neno la Mungu linatwambia ya kwamba dunia yote "ilijaa dhuluma." Watu walikuwa wakisema uwongo, wakiiba, waki-pigana, na wakiuana. Kusema kweli, mambo yote waliyofanya yalikuwa maovu kwa saba-bu fikira zao zilikuwa mbaya.

Mungu amemwumba mwanadamu na kumpa ulimwengu mzuri wa kukaa. Je! unafikiri Mungu aliwaza nini wakati alipoona karibu kila mtu akimwacha na kufuata njia yake mwenyewe na kuishi maisha mabaya? Mungu alihuzunika sana. Alisema ya kuwa angea-ngamiza viumbe vyote alivyoumba.

Lakini kulikuwa na mtu mmoja ambaye alimpendeza Bwana. Mtu huyu aliitwa Nuhu. Biblia inasema, "Nuhu akapata neema macho-ni pa Bwana." (Mwanzo 6:8)

Nuhu, kama watu wote waliozaliwa baada ya Adamu, alikuwa mwenye dhambi

kwa hiyo alistahili kufa. Lakini kulingana na Biblia, Nuhu alitaka kufanya mambo yale tu ambayo alijua ya kwamba Mungu alimtaka kufanya. Alikwenda pamoja na Mungu. Maana yake ni kwamba, alisema na Mungu mara kwa mara katika maombi na alimtii.

Siku moja, Mungu alimwambia Nuhu ya kwamba angeharibu nchi pamoja na watu kwa sababu watu waliijaza nchi kwa dhuluma na maovu. Lakini alimwahidi Nuhu ya kwamba yeye pamoja na jamaa yake hawangeangamia. Mungu alimwambia Nuhu jambo la kufanya. Alimtaka kufanya safina (meli). Nuhu hakujua jinsi ya kufanya safina, lakini hakuhitaji kujua kwa sababu Mungu alimwambia mambo yote ya kufanya.

Hebu tuone kama wewe na wanafunzi wenzako mnaweza kufanya mchezo wa kuigiza mambo yaliyomfanyikia Nuhu. (Nuhu anakata mti. Kisha rafiki anakuja.)

Rafiki: Jambo Nuhu. Je! unafanya nini?

Nuhu: Sijambo. Nakata miti ya kufanya safina.

Rafiki: Safina! Kwa nini unataka kufanya safina? Wewe hukai karibu na bahari. Wala hakuna hata ziwa au mto karibu hapa. Je! safina hiyo utaitumia wapi? (Anacheka.)

Nuhu: Ninafanya safina kwa sababu Mungu aliniambia nifanye. Alisema ya kwamba ataharibu ulimwengu kwa sababu umejaa dhambi. Uso

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

wote wa nchi utafunikwa na maji, na watu wale tu watakao-kuwa ndani ya safina ndio watakaosalimika. Kama ukimwamini Mungu na kuhuzunika kwa ajili ya dhambi zako, atakuokoa wewe pia.

Rafiki: (Anacheke.) Je! una maana gani kwa kusema ati nihuzunike kwa ajili ya dhambi zangu? Mimi ni mtu mwema. Bila shaka, Nuhu, umgonjwa. Ni miti gani hiyo unayokata?

Nuhu: Ni miti ya mvinje kwa sababu ndiyo namna ya miti ambayo Mungu aliniambia kutumia. Pia aliniambia jinsi ukubwa wa safina hiyo ungekuwa, na jinsi ya kufunika ndani na nje kwa lami, kisha maji hayataweza kuingia ndani.

(Marafiki wengine wanakuja.)

Rafiki wa 1: Tazameni kitu Nuhu anachokifanya. Anafanya safina.

Rafiki wa 2: Safina! Una nini, wewe Nuhu? Unapoteza bure wakati wako na miti! (Anamcheke Nuhu.)

Nuhu: Mkimwamini Mungu na kusikitika kwa ajili ya dhambi zenu, mtaokolewa wakati Mungu atakapoharibu nchi.

Marafiki: Wote wanamcheka Nuhu kwa sauti. Nuhu anaendelea kufanya safina na hatimaye anamaliza. Kisha anaanza kukusanya kila namna mbili za wanyama, mume na mke na kuwatia ndani ya safina. Marafiki wale wanamwangualia Nuhu na kumcheka, lakini Nuhu hajali kucheka kwao. Anajaribu kuwahubiria lakini hawamsikilizi.

Nuhu: Mke wangu, njoo ndani ya safina. Nimekwisha kuweka wanyama wawili wa kila namna ndani ya safina kama Mungu alivyosema. Sasa ni wakati wetu kuingia. Wanangu, waleteni wake zenu ili sote tuingie ndani ya safina ili tuweze kuokoka wakati Mungu atakapoiharibu nchi.

Marafiki: (Wanacheka lakini wengine wanaanza kustaaajabu kama jambo hilo lingekuwa kweli.)

Nuhu: Hebu tuhakikishe kama tumefanya mambo yote ambayo Mungu alisema. Hatutaki kuacha kufanya jambo hata moja. Tumekwisha kuwachukua wanyama wawili wa kila namna, na tumekwisha kuweka chakula cha kututosha sisi na wanyama wetu ndani safina. Ndiyo, tumekwisha kufuata maongozi ya Mungu katiika kila jambo. Ninyi marafiki, kama mtatubu dhambi zenu, na kumwamini Mungu, atawaokoa.

Marafiki: (Wote wanacheka.)

(Nuhu anawaingiza jamaa yake yote ndani ya safina, kisha naye anaingia ndani. Wakiwa humo ndani, wanangojea wakijua ya kwamba baada ya muda mfupi mvua itaanza kunyesha sana. Lakini watu waliokuwa nje ya safina bado hawakumsikiliza Nuhu. Lakini Nuhu alikuwa na furaha kwa sababu alikwisha kufanya mambo yote ambayo Mungu alimwambia kufanya. Mungu alisema ya kwamba baada ya siku saba mvua ingeanza kunyesha kwa muda wa siku arobaini mchana na usiku. Nuhu alingojea.)



KAZI YA KUFANYA:

Miaka mingi baada Kaini kumwua nduguye, karibu kila mtu duniani alikuwa mwovu. Ni fikira gani ambazo Mungu aliendelea kuona mioyoni mwa watu?

Soma Mwanzo 6:8-10 uone kwamba Nuhu alikuwa mtu wa namna gani. Chora mistari kutoka kwa picha ya Nuhu hadi kwa maneno ya kweli yanayozungumza habari zake.



Nuhu alimpendeza Bwana.

Nuhu alikuwa mtu wa haki.

Nuhu alikwenda pamoja na Mungu.

Nuhu alikaa katika Bustani ya Edeni.

Wana watatu wa Nuhu walikuwa Shemu, Hamu, na Yafeth.

Nuhu alikuwa pia na mabinti watatu.

Jibu maswali yafuatayo.

Je! Nuhu aliambiwa na Mungu kutumia mti wa namna gani kufanya safina?

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

Je! Nuhu alijua kwa jinsi gani kufanya safina? _____

Mungu alimwambia Nuhu kufunika nini ndani na nje ya safina ili maji yasiingie? _____

Je! safina hiyo ingekuwa na urefu wa mikono mia ngapi? _____

Urefu wa mkono mmoja ulikuwa kama futi 1½. Kwa hiyo safina ingekuwa na urefu wa futi ngapi? _____

Piga mstari chini ya njia mojawapo ambayo Mungu angetumia kuharibu nchi na vitu vyote vilivyokuwa ndani.

Kwa moto

Kwa gharika

Kwa vita

Kwa tete-
meko la
ardhi.

Kwa njaa

Kwa mago-
njwa.

Piga mstari chini ya majina ya watu ambao Mungu alipanga kuokoa ndani ya safina wakati angemwangamiza kila mtu.

Nuhu na mkewe

Mabinti wa Nuhu
na mabwana zao.

Ndugu ya Nuhu

Wana wa Nuhu na
wake zao.

Mungu alimwambia Nuhu kuchukua wanya-
ma na vifaa vingine na kuweka ndani ya
safina. Je! Nuhu alitimiza sehemu tu au

alifanya mambo yote ambayo Mungu aliamuru? _____

Hatimaye, wakati wa kupakia safina ulifika. Soma maagizo ya Mungu ya mwisho katika Mwanzo 7:1-5. Nuhu aliweka wanya-ma ndani, na aliwaambia jamaa yake kuingia.

Je! mvua ingeanza kunyesha baada ya siku ngapi? _____

Je! mvua ingenyesha kwa siku ngapi usiku na mchana? _____

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Nuhu akafanya kama vile Bwana alivyomwamuru." Mwanzo 7:5

Je! siku ya leo, ulisoma Neno la Mungu?

Ulimwonyesha Mungu ya kwamba unaamini mambo unayoyasoma kwa kumtii?

MANENO YA KUJIFUNZA:

gharika.....furiko la maji.
safina.....chombo kama jahazi.
mvinje.....mti mrefu sana, matunda
yake madogo, na majani
yake kama nyuzi za shada.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Mwanzo 6:5-7:5

BWANA akaona ya kuwa maovu ya mwana-damu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu

sikuzote. (6) BWANA akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani, akahuzunika moyo. (7) BWANA akasema, Nitamfutilia mbali mwanadamu niliyemwumba usoni pa nchi; mwanadamu na mnyama, na kitambaacho na ndege wa angani; kwa maana naghairi ya kwamba nimewafanya. (8) Lakini Nuhu akapata neema machoni pa BWANA.

(9) Hivi ndivyo vizazi vya Nuhu. Nuhu alikuwa mtu wa haki, mkamilifu katika vizazi vyake; Nuhu alikwenda pamoja na Mungu. (10) Nuhu akazaa wana watatu wa kiume, Shemu, na Hamu, na Yafethi. (11) Dunia ikaharibika mbele za Mungu, dunia ikajaa dhuluma. (12) Mungu akaiona dunia, na tazama, imeharibika; maana kila mwenye mwili amejiharibia njia yake duniani.

(13) Mungu akamwambia Nuhu, Mwisho wa kila mwenye mwili umekuja mbele zangu; kwa sababu wameijaza dunia dhuluma, basi nitawaharibu pamoja na dunia. (14) Ujifanyie safina ya mti wa mvinje; fanya na vyumba ndani ya safina, ukaifunike ndani na nje kwa lami. (15) Hivi ndivyo utakavyoifanya; mikono mia tatu urefu wa safina, mikono hamsini upana wake, na mikono thelathini kwenda juu kwake. (16) Uifanyie safina mwangaza, ukaumalize juu kiasi cha mkono mmoja; ukautie mlango wa safina katika ubavu wake; ukaifanyie dari tatu, ya chini, ya pili, na ya tatu. (17) Na tazama, nitaleta gharika ya maji juu ya nchi, niharibu kila kitu chenye mwili na pumzi ya uhai, kisiwepo chini ya mbingu; kila kilichoko duniani kitakufa. (18) Lakini nitaifanya agano langu nawe kuwa thabiti; nawe utaingia katika safina, wewe, na wanao, na mkeo, na wake za wanao, pamoja nawe. (19) Na katika

kila kilicho hai chenye mwili, wawili wa kila namna utawaleta ndani ya safina, kuwahifadhi pamoja nawe; wawe mume na mke. (20) Katika vyote virukavyo kwa jinsi yake, na kila namna ya mnyama kwa jinsi yake, kila kitambaacho juu ya nchi kwa jinsi yake, wawili wa kila namna watakuja kwako, ili uwahifadhi. (21) Ukajitwalie chakula cha kila namna kina-cholika, ukakusanye, nacho kitakuwa ni chakula chenu na chao. (22) Ndivyo alivyofanya Nuhu, sawasawa na vyote alivyomwamuru Mungu, hivyo ndivyo alivyofanya.

7:1-5

BWANA akamwambia Nuhu, Ingia wewe na jamaa yako yote katika safina; kwa maana nimekuona wewe u mwenye haki mbele zangu katika kizazi hiki. (2) Katika wanyama wote walio safi ujitwalie saba saba, mume na mke; na katika wanyama wasio safi wawili wawili, mume na mke. (3) Tena katika ndege wa angani saba saba, mume na mke; ili kuhifadhi hai mbe-gu juu ya uso wa nchi yote. (4) Kwa maana baada ya siku saba nitainyeshea dunia mvua, siku arobaini mchana na usiku; na kila kilicho hai nilichokifanya juu ya uso wa nchi nitakifutilia mbali. (5) Nuhu akafanya kama vile BWANA alivyomwamuru.

UPINDE HUFUATA GHARIKA

MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo 7:6-8:22;
9:12-19

Siku saba kabla Mungu kuleta gharika, alimwambia Nuhu kuwachukua jamaa yake na wanyama wawili wa kila namna na kuwaingiza ndani ya safina. Nuhu alihitaji siku hizo saba kuwaleta wanyama wote na chakula na vifaa vingine na kuviingiza ndani ya safina. Je! unafikiri marafiki za Nuhu walifikiri nini wakati walipomwona akiingia ndani ya safina? Unadhani ya kwamba walikumbuka maonyo yale ambayo Nuhu aliwapa kila mwaka wakati alipokuwa akifanya safina?

La, waliendelea tu kuishi kana kwamba Mungu hakuwaonya ya kuwa wangeadhibiwa kama wangeendelea kutomjali.

Katika wiki ile kabla ya gharika, hakukuwa na dalili yo yote ya kuonyesha kwamba mvua ingenyesha na kufunika uso wa nchi yote. Onyo la pekee ambalo Nuhu alikuwa nalo lilikuwa lile ambalo Mungu alimpa. Mungu alikuwa amemwambia ya kwamba baada ya siku saba mvua ingeanza kunyesha. Nuhu alitosheka na onyo hili. Alimwamini Mungu.

Je! ni watu wangapi waliingia ndani ya safina? Watu wanane. Watu hao walikuwa Nuhu, mkewe, wanawe watatu na wanawake zao. Pia Nuhu alichukua wanyama wawili (mume na mke) wa kila namna na kuwaingiza ndani ya safina kama Mungu alivyomwambia

kufanya. Safina ilikuwa na mlango mmoja tu na kila kiumbe ambacho kingeingia ndani ilikuwa ni lazima kupitia mlango ule. Wakati wanyama na watu wale wanane ambao Mungu aliwataka kuwa ndani ya safina walipokwisha kuingia, Bwana mwenyewe aliufunga mlango ule.

Baada ya mlango ule kufungwa hakuna mtu hata mmoja aliyekuwa nje ya safina ambaye angeweza kuingia ndani. Na watu waliokuwa ndani ya safina walikuwa salama wakilindwa na Mungu mwenyewe.

Siku saba baada ya Mungu kumwamuru Nuhu kuingia ndani ya safina, mvua ilianza kunyesha. Tuendeleo kuiga hadithi ya Nuhu kama tulivyoianza katika somo lili-lopita.

Mchezo: (Nuhu na jamaa yake wako salama ndani ya safina. Marafiki zao wote wako nje ya safina.)

Rafiki wa 1: Ni mvua gani hii inayonyesha kutoka mbinguni?

Rafiki wa 2: Sijui, sijapata kuona mvua kama hii.

Rafiki wa 3: Nuhu alisema ya kwamba Mungu angeharibu nchi kwa maji. Mnafikiri alisema ukweli?

Rafiki wa 1: Labda alisema ukweli. Hebu tujaribu kumwuliza kuturu-husu kuingia ndani ya safina.

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

Marafiki hao wote pamoja: Ndiyo, tutaingia ndani ya safina sasa. (Wanakwenda kwa safina lakini wanakuta kama mlango wake umefungwa na hawawezi kuingia ndani. Mungu mwenyewe ndiye ameufunga mlango ule.)

Rafiki wa 1: Tutafanya nini? Hatuwezi kuingia ndani ya safina. Tutakufa.

(Wote wanahuzunika wanapotambua kwamba watakufa.)

MWISHO

Mvua iliendelea kunyesha, na maji yakazidi kujaa. Biblia inasema kwamba, "Chemchemi zote za vilindi vikuu zilibubujika". (Mwanzo 7:11) Sasa ndipo watu walipoamini onyo la Mungu lakini walikuwa wamechelewa.

Labda wengi wao walikimbilia vilele vya milima mirefu wakifikiri kwamba hawangekufa. Lakini maji yalipozidi kujaa juu ya nchi, wote walinaswa. Baada ya siku chache, maji yalifunikiza kabisa milima, na wale wote waliopanda milima hiyo wakitaka usalama walizama.



Hatimaye vilele vya milima yote mirefu vilifunikizwa na maji, kisha maji yakapanda juu yao kiasi cha futi ishirini. Kila kitu kilikufa isipokuwa samaki na wanyama wengine wa bahari.

Lakini ni nini kilichofanyika kwa safina wakati maji yalipofunika nchi? Ingawa maji yalijaa sana, safina ilielea tu juu. Nyumba zote ziliharibiwa, lakini nyumba moja (yaani, safina) ambayo Mungu alimwambia Nuhu kuijenga, sasa ilikuwa ikiwalinda yeye (Nuhu) na jamaa yake na wanyama wao na kuwaweka katika hali ya joto. Nuhu alifurahi ya kwamba alifanya kila kitu ambacho Mungu alimwambia kufanya.

Mvua iliacha kunyesha baada ya siku arobaini, lakini maji yalifunika uso wote wa nchi kwa miezi mitano. Hatimaye safina ilitua juu ya milima ya Ararati. Upepo sasa ulivuma juu ya nchi, maji yakapungua. Maji yaliendelea kupungua pole pole. Miezi mitatu baadaye, vilele vya milima mirefu viliweza kuonekana.

Ikawa baada ya siku arobaini, Nuhu alimtwaa Kunguru, ndege mwenye nguvu, akamtuma nje. Kunguru huyo aliruka kwa muda mrefu sana. Nuhu alingojea, lakini kunguru hakurudi. Kisha Nuhu alitwaa njiwa, ndege mdhaifu, akamtuma nje. Njiwa hakupata mahali pa kutua kupumzika, kwa hiyo alimrudia Nuhu safinani. Nuhu alingojea kwa siku nyingine saba, kisha akamtuma njiwa tena. Jioni ile njiwa alimjia akiwa na jani bichi la mzeituni kinywani mwake. Hii ilimwonyesha Nuhu ya kwamba

maji yalikuwa yakipungua lakini ndege yule hakupata mahali pa kukaa.

Baada ya siku nyingine saba, Nuhu alimtuma njiwa tena kwa mara ya tatu. Wakati huu njiwa hakurudi. Maji yalikuwa yamekwisha kupungua sana hata akapata mahali pa kujenga kiota chake, akakaa. Baada ya siku kadha, Nuhu aliondoa kifuniko cha safina, akaona uso wa nchi ukiwa umekauka. Lakini hakutoka ndani ya safina kwa muda karibu miezi miwili. Mungu alimtaka kukaa ndani ya safina mpaka mabonde yote yangekauka.

Mungu alimwambia Nuhu kutoka katika safina pamoja na jamaa yake na wanyama wote. Bila shaka walifurahi. Wanyama walitoka katika safina, wakakimbia mara moja pande zote wakitafuta mahali papya pa kukaa.

Je! ni kitu kipi cha kwanza ambacho Nuhu alifanya wakati Mungu alipomtoa katika safina? Nuhu alimshukuru Mungu kwa kuwaokoa yeye na jamaa yake kutokana na gharika, akamtolea Mungu sadaka madhabahuni.

Nuhu alipendezwa sana na sadaka ya Nuhu, akaahidi kwamba hangeharibu nchi tena kwa gharika.

Kisha Mungu aliweka upinde kama ishara yake kwamba ahadi yake ya kutoharibu nchi kwa gharika hangeibadili milele. Sasa Nuhu hangehitaji kuogopa wakati mvua ingenyesha tena.



KAZI YA KUFANYA:

Baada ya Mungu kuongoza jamaa ya Nuhu kuingia ndani ya safina, alifanya mvua kubwa kunyesha. Je! mvua hiyo ilinyesha siku ngapi? _____

Soma Mwanzo 8:1-5 na kuandika namba (1, 2, 3, na kuendelea) kando ya sentensi hizi nne kulingana na wakati yalipotukia.

- Katika mwezi wa saba safina ilitua juu ya milima ya Ararati.
- Mungu alivumisha upepo juu ya nchi.
- Vilele vya milima vilionekana katika mwezi wa kumi.
- Mwisho wa siku mia na hamsini maji yakapunguka.

Nuhu alitumia ndege wa namna mbili kumwezesha kujua wakati ambapo maji yalipungua juu ya nchi. Baada ya siku arobaini, Nuhu alituma ndege wa kwanza nje kuona kama gharika ilikwisha.

Je! ndege huyo alikuwa yupi? _____


Je! ndege huyo alirudi? _____

Kwa sababu ndege kama huyo hula mizoga, Nuhu alijua kwamba angeweza kukaa nje ya safina. Kisha Nuhu alituma ndege mwingine kumfahamisha juu ya gharika.

Je! Nuhu alituma ndege gani wakati huu? _____

Nuhu alimtuma ndege huyu mara ngapi?

Eleza kwa maneno yako mwenyewe jambo lilihofanyika kila wakati ambapo njiwa alitumwa.



Hatimaye Nuhu na jamaa yake walitoka katika safina. Nuhu hakusahau kumshukuru Mungu kwa kuwaokoa yeye na jamaa yake.

Je! Nuhu alimtolea Mungu sadaka ya namna gani? _____

Kisha Mungu alifanya agano la ajabu. Je! Mungu alisema hangelaani nini tena? _____

Je! Mungu aliahidi kwamba hangeua nini tena?

Je! Mungu alitoa ishara gani kuwakumbusha watu wake juu ya ahadi yake?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Mimi ndimi mlango; mtu akiingia kwa mimi, ataokoka."

Yohana 10:9

Je! ni njia ipi ya pekee iliyokuwa ya kuingia safinani?

Ni watu wale tu walioingia katika njia ile ndio waliookolewa. Wengine wote waliokaa nje ya safina waliangamia.

Katika kifungu chako cha kukumbuka Bwana anasema kuwa yeye ni nini?

Yesu ndiye njia ya pekee ya kuingia mbinguni. Na wale tu wanaomjia Mungu kwa njia ya Yesu ndio wanaokolewa katika dhambi zao.

MANENO YA KUJIFUNZA:

mzoga.....mwili wa mnyama aliye-kufa.

Kunguru.....ndege mweusi mwenye paku jeupe shingoni, wengine ni weusi mwili mzima

Njiwa.....ndege mdogo kama hua

upinde.....tao la rangirangi lina-loonekana mbinguni pengine wakati wa mvua.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Mwanzo 7:6-8:22; 9:12-19

Naye Nuhu alikuwa mtu wa miaka mia sita hapo hiyo gharika ya maji ilipokuwa juu ya nchi. (7) Nuhu akaingia katika safina, yeye, na wanawe, na mkewe, na wake za wanawe pamoja naye; kwa sababu ya maji ya gharika. (8) Na katika wanyama walio safi, na wanyama wasio safi, na ndege, navyo vyote vitambaavyo juu ya nchi, (9) wakaingia katika safina alimo Nuhu, wawili wawili, mume na mke, kama vile Mungu alivyomwamuru Nuhu. (10) Ikawa baada ya siku hizo saba, maji ya gharika yakawa juu ya nchi. (11) Katika mwaka wa mia sita wa maisha ya Nuhu, mwezi wa pili, siku ya kumi na saba ya mwezi, siku ile chemchemi zote za vilindi vikuu zilibubujika kwa nguvu, madirisha ya mbinguni yakafunguka. (12) Mvua ikanyesha juu ya nchi, siku arobaini mchana na usiku. (13) Siku ile ile Nuhu akaingia katika safina, yeye, na Shemu na Hamu na Yafethi, wana wa Nuhu, na mkewe Nuhu, na wake watatu wa wanawe pamoja naye; (14) wao na kila mnyama wa mwitu kwa jinsi yake, na kila mnyama wa kufugwa kwa jinsi yake, na kila kitambaacho, chenye kutambaa juu ya nchi, kwa jinsi yake, na kirukacho kwa jinsi yake, kila ndege wa namna yo yote. (15) Waliingia katika safina alimo Nuhu, wawili wawili, wa kila chenye mwili kili-cho na pumzi ya uhai ndani yake. (16) Na walioingia, waliingia mume na mke, wa kila kitu chenye mwili, kama vile alivyo-mwamuru Mungu; BWANA akamfungia.

(17) Ile gharika ilikuwako juu ya nchi siku arobaini; nayo maji yakazidi,

yakaeleza safina, ikaelea juu ya nchi.

(18) Maji yakapata nguvu, yakazidi sana juu ya nchi; na ile safina ikaelea juu ya uso wa maji. (19) Maji yakapata nguvu sana juu ya nchi; na milima mirefu yote iliyokuwako chini ya mbingu ikafunikizwa. (20) Maji yakapata nguvu, hata ikafunikwa milima kiasi cha mikono kumi na mitano. (21) Wakafa wote wenye mwili waendao juu ya nchi, na ndege, na wanyama wa kufugwa, na kila mnyama wa mwitu, na kila kitamba-acho chenye kutambaa juu ya nchi, na mwanadamu; (22) kila kitu chenye pumzi ya roho ya uhai puani mwake kikafa, kila kilichokuwako katika nchi kavu. (23) Kila kilicho hai juu ya uso wa nchi kikafuti-liwa mbali tangu mwanadamu hata mnyama wa kufugwa, na kitambaacho, na ndege wa angani; vilifutiliwa mbali katika nchi, akabaki Nuhu tu, na hao walio pamoja naye katika safina. (24) Maji yakapata nguvu juu ya nchi siku mia na hamsini.

8:1-22

Na Mungu akamkumbuka Nuhu, na kila kilicho hai, na wanyama wote waliokuwamo pamoja naye katika safina; Mungu akavumi-sha upepo juu ya nchi, maji yakapungua; (2) chemchemi za vilindi zikafungwa, pia na madirisha ya mbinguni, mvua kutoka mbinguni ikazuiliwa; (3) maji yakadumu kuondoka katika nchi; na mwisho wa siku mia na hamsini maji yakapunguka. (4) Mwezi wa saba, siku ya kumi na saba ya mwezi, safina ikatua juu ya milima ya Ararati. (5) Maji yakapunguka-punguka hata mwezi wa kumi; mwezi huo wa kumi, siku ya kwa-nza ya mwezi, vilele vya milima vikaonekana. (6) Ikawa baada ya siku arobaini,

Nuhu akalifungua dirisha la safina, alilolifanya; (7) akatoa kunguru, naye akatoka akaenda huko na huko, hata maji yaka-kauka juu ya nchi. (8) Kisha akatoa njiwa, aone kwamba maji yamepunguka usoni pa nchi; (9) bali yule njiwa hakuona mahali pa kutua kwa wayo wa mguu wake, akamrudia Nuhu safinani, maana maji yalikuwa juu ya uso wa nchi yote; naye akanyosha mkono, akamtwaa, akamwingiza mle safinani.

(10) Akangoja na siku saba tena; kisha akamtoa yule njiwa katika safina mara ya pili, (11) njiwa akamjia jioni, na tazama, alikuwa na jani bichi la mze-ituni kinywani mwake, ambalo amelitunda, basi Nuhu akajua ya kwamba maji yamepungu-ka juu ya nchi. (12) Akangoja na siku saba tena, akamtoa yule njiwa; naye asimrudie tena kamwe.

(13) Ikawa mwaka wa mia sita na moja, mwezi wa kwanza, siku ya kwanza ya mwezi, maji yalikauka juu ya nchi. Nuhu akaondoa kifuniko cha safina, naye akaona, na tazama, uso wa nchi umekauka. (14) Na mwezi wa pili, siku ya ishirini na saba ya mwezi, nchi ilikuwa kavu.

(15) Mungu akamwambia Nuhu, akisema, (16) Toka katika safina, wewe, na mkeo, na wanao, na wake za wanao pamoja nawe. (17) Utoe pamoja nawe kila kilicho hai kilichomo pamoja nawe, chenye mwili, ndege, na mnyama, na kila kitambaacho, chenye kutambaa juu ya nchi; wajae katika nchi, wawe na uzazi, wakaongezeke katika nchi. (18) Basi Nuhu akatoka, yeye, na wanawe, na mkewe, na wake za wanawe pamoja naye; (19) kila mnyama, na kila kitambaacho, na kila ndege, kila kinachokwenda juu ya nchi kwa kabila zao, wakatoka

katika safina. (20) Nuhu akamjengea BWANA madhabahu; akatwaa katika kila mnyama aliye safi, na katika kila ndege aliye safi, akavitoa sadaka za kuteketezwa juu ya madhabahu. (21) BWANA akasikia harufu ya kumridhisha; BWANA akasema moyoni, Sitailaani nchi tena baada ya hayo kwa sababu ya wanadamu, maana mawazo ya moyo wa mwanadamu ni mabaya tangu ujana wake; wala sitapiga tena baada ya hayo kila kilicho hai kama nilivyofanya. (22) Muda nchi idumupo, majira ya kupanda, na mavuno, wakati wa baridi na wakati wa hari, wakati wa kaskazi na wakati wa kusi, mchana na usiku, havitakoma.

9:12-19

Mungu akasema, Hii ndiyo ishara ya agano nifanyalo kati yangu na ninyi, na kila kiumbe hai kilichoko pamoja nanyi, kwa vizazi vyote hata milele; (13) Mimi nauweka upinde wangu winguni, nao utakuwa ni ishara ya agano kati yangu na nchi. (14) Hata itakuwa nikitanda mawingu juu ya nchi, upinde utaonekana winguni, (15) nami nitalikumbuka agano langu, lililoko kati yangu na ninyi, na kila kiumbe hai katika wote wenye mwili, wala maji hayatakuwa gharika tena kuwaharibu wote wenye mwili. (16) Basi huo upinde utakuwa winguni; nami nitauangalia, nipate kuli-kumbuka agano la milele lililoko kati ya Mungu na kila kiumbe hai katika wote wenye mwili kilichoko katika nchi. (17) Mungu akamwambia Nuhu, Hii ndiyo ishara ya agano nililoliweka kati yangu na wote wenye mwili walioko katika nchi.

(18) Wana wa Nuhu waliotoka katika safina, ni Shemu, na Hamu, na Yafethi;

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

na Hamu ndiye baba wa Kanaani. (19) Hawa watatu walikuwa wana wa Nuhu; na kwa hao nchi yote ikaenea watu.


MUNGU ASEMA NA MWANADAMU

MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo 11:27-12:9

Mungu aliwataka watu kumpenda. Ali-taka waseme naye lakini wao hawakuonekana kama walimpenda. Hawakuonekana kama wali-taka kusema naye. Walikuwa kama watu waliokufa.

Hivi ndivyo watu walivyoishi kabla ya gharika. Hivi pia ndivyo watu walivyo-ishi baada ya gharika.

Jamaa ya Nuhu iliongezeka. Wanawe wale watatu pia walizaa watoto. Wakati nchi ile iliyokuwa karibu na milima ya Ararati ilipojaa, watu walihamia upande wa kusini katika iliyokuwa katikati ya mito miwili mikubwa, mto Hidekeli na mto Frati. Je! unaweza kupata mito hii miwili katika ramani?



Makundi ya watu hawa walikaa Babeli. Walivumbua jinsi ya kujenga nyumba za mawe. Watu hawa walikuwa jamaa ya Shemu, mmojawapo wa wana wa Nuhu. Mji mmoja walioujenga uliitwa Uru wa Wakaldayo. Ulikuwa katika nchi ya Wakaldayo, nchi

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

ambayo mito ile miwili ilikutana. Je!
unaweza kuona Uru katika ramani yako?

Uru ulikuwa mji mkuu. Watu wengi waliokaa ndani walikuwa matajiri. Lakini hawakumpenda Bwana. Waliabudu mwezi. Kwa kujaribu kumfanya mungu wao kuwa halisi kwao, walifanya sanamu zake ndogo ndogo. Waliabudu sanamu hizi.

Miaka kama 400 hivi baada ya gharika, mtu mmoja aliyeitwa Abramam alikaa katika mji ule wa Uru. Babaye Abramam na majirani zao wote waliabudu sanamu, lakini hatujui habari juu ya Abramam. Siku moja, Abramam alichukua vitu vyake vyote, akatoka katika nchi yake. Bila shaka ilikuwa vigumu sana kwa watu kufahamu ni kwa nini Abramam aliacha mji wao wenye mafanikio na kute-mbea maili nyingi kwenda kukaa katika nchi ya malisho tu. Lakini Mungu ndiye aliyemwambia kutoka katika nchi yake na kuwaacha jamaa zake na nyumba yake baba yake na kwenda kukaa katika nchi ambayo Mungu angemwonyesha.

Ikiwa Abramam hakumjua Mungu kabla ya wakati huu, basi, bila shaka Mungu alimwonyesha sasa ya kwamba yeye ndiye aliyekuwam Mungu mmoja wa kweli. Abramam alikuwa na nia kamili ya kutoka katika nchi aliyozaliwa na kuwaaga marafiki zake na kwenda katika nchi ya kigeni. Abramam alimtii Mungu bila kuuliza swali lo lote. Aliwachukua Sarai mkewe, Tera babaye, na Lutu mtoto wa nduguye.



Wakati Abramu alipotoka nyumbani kwao katika mji wao wa Uru, hakujua kama angesafiri umbali gani kabla ya kufika katika nchi ambayo Mungu alimtaka kwenda. Iliwabidi kutembea pole pole kwa miguu au kwa kupanda punda au ngamia. Walisafiri maili 800 kando kando ya Mto Frati miaka wakafika mahali palipoitwa Harani, katika nchi ya Mesopotamia. Je! ulitafuta mji huo wa Harani katika ramani yako? Abramu na wenzake walipiga kambi yao Harani mpaka wakati Tera, baba yake, alipokufa.

Baada ya kifo cha Tera, Bwana alisema na Abramu tena. Alimwambia kuondoka Harani kwenda katika nchi ambayo angemwonyesha. Wakati huu Mungu aliagana na Abramu ahadi saba. Ahadi hizo ni kama ifuatavyo:

1. Nitakufanya kuwa taifa kubwa. (Taifa hili ndilo lililokuwa la Waebrania. Wao wote walikuwa uzao wa Abramu.)

2. Nitakubariki. (Siku chache zijazo tutaona jinsi Mungu alivyombariki Abramam wakati tutakaposoma juu ya maisha yake. Abramam ndiye mtu wa pekee katika Biblia anayeitwa "rafiki ya Mungu.")
3. Nitalikuza jina lake. (Jina la Abramam linaheshimiwa sana na Wayahudi kwa sababu yeye ni baba ya taifa lao. Jina lake pia linaheshimiwa sana na Wakristo ambao humwita baba ya kiroho ya waamini wote.)
4. Utakuwa baraka. (Abramam alikuwa baraka, lakini si kwa jamaa yake pekee yake, bali ni kwa vizazi vyote vya baadaye, kwa sababu katika yeye na katika jamaa yake na taifa lake, ndipo alipozaliwa Mwokozi wa Ulimwengu, Bwana Yesu Kristo.)
5. Nitawabariki wakubarikio. (Ahadi hii bado iko mpaka sasa. Mungu atawabariki wale wanaowabariki watoto wake.)
6. Nitamlaani akulaaniye. (Mungu aliahidi pia ya kwamba atawalaani wakatili na watu wasiowatendea watu wake haki.)
7. Katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa. (Kristo alizaliwa katika jamaa ya Abramam. Tunaweza kuona kwa urahisi jinsi kuja kwa Kristo kumeleta baraka kwa jamaa

MUNGU ASEMA NA MWANADAMU

zote za Kikristo. Wakati wo wote ambapo Kristo huhubiriwa, watu hubarikiwa.)

Ingawa Abramumu alianza kuwa mzee, bado hakuacha kusafiri. Wakati wo wote ambapo Mungu alimwambia kuhama, alihama. Yeye pamoja na jamaa yake waliondoka Harani wakasafiri maili 500 kwenda upande wa kusini magharibi, wakipitia milimani na kuvuka mito. Hatimaye walifika Kanaani, nchi ambayo Mungu aliwachagulia. Nchi hiyo baadaye iliitwa Israeli kwa jina la (Yakobo) mjukuu wa Abramumu. Kwa sababu Yesu alifanya kazi pale wakati alipokuwa duniani, nchi hiyo imekuwa ikiitwa "Nchi Takatifu."

Mahali pa kwanza ambapo Abramumu alisimama katika nchi ya Kanaani paliitwa Shekemu. Katika mahali hapo ndipo Mungu alipompa Abramumu ahadi kuu. Mungu aliahidi kuwapa wana wa Abramumu nchi hiyo ya Kanaani. Kisha Abramumu alimjengea Mungu madhabahu. Alimwabudu Mungu na kumshukuru kwa ahadi hiyo yake kuu.

Abramumu hakujenga nyumba mahali pamoja. Alihamisha hema yake kila mahali. Kila mahali alikokwenda alikumbuka kumjengea Mungu madhabahu ambapo alimtolea sadaka ya kuteketezwa na kumwabudu kama alivyomfundisha.

KAZI YA KUFANYA:

Soma juu ya mwaliko wa Mungu kwa Abramumu. Piga mstari chini maneno yote ya

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

kumalizia ambayo ni ya kweli.

Mungu alimwambia Abramam kutoka katika

nchi yake utajiri jamaa

nyumba ya babaye

Mungu alimwambia Abramam kwenda

Mesopotamia Afrika Misri

katika nchi ambayo angemwonyesha

Abramam alichukua

mkeve mamaye dadaye

babaye mtoto wa nduguye

rafikiye

Abramam alitoka nyumbani kwao bila
kujua mahali ambapo alikuwa akienda.
Chora mistari kutoka kwa maneno yaliyo
upande wa kushoto hadi kwa yale yaliyo
upande wa kulia ambayo yanayakamilisha.

Tera alikuwa

mkeve Abramam

Lutu alikuwa

Harani

Sarai alikuwa

babaye Abramam

Tera alikufa

mtoto wa ndugu
ya Abramam

MUNGU ASEMA NA MWANADAMU

Tazama ramani yako. Chora mviringo kwa mji ambao Abramam alikaa wakati Mungu aliposema naye kwa mara ya kwanza. Sasa chora njia ambayo alifuata akisafiri.

Mungu aliagana na Abramam ahadi 7. Kamilisha ahadi hizi:

1. Nitakufanya kuwa taifa_____.
2. Nita_____.
3. _____ jina lako.
4. Utakuwa _____.
5. Nitawabariki_____.
6. Nitamlaani_____.
7. Katika wewe jamaa zote za dunia
_____.

Hatimaye Abramam alifika katika nchi ya Kanaani. Je! alipofika huko alijenga nini? Andika neno KWELI katika mstari ulio mbele ya jengo ambalo tunaambiwa Abramam alijenga katika Kanaani.

shule_____

hospitali_____

nyumba_____

madhabahu_____

Je! alifanya hivyo kwa nini?_____

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Yeye aliye wa Mungu huyasikia maneno ya Mungu."
Yohana 8:47

Je! wewe hujifanya kwamba husikii wakati mama yako anapokuita? Watu wengine hawasikilizi maneno ya Mungu. Kusikia maneno ya Mungu maana yake ni kufahamu jambo analotaka ufanye. Ni wale tu walio wa Mungu ndio wanaoweza kufahamu kweli jambo ambalo Mungu anataka wao kufanya. Je! unasikia maneno ya Mungu moyoni mwako?

MANENO YA KUJIFUNZA:

katili.....asiye na huruma, mdhalimu, mwovu

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Mwanzo 11:27-12:9

Na hivi ndivyo vizazi vya Tera. Tera akamzaa Abram, na Nahori, na Harani. Harani akamzaa Lutu. (28) Harani akafa kabla ya baba yake Tera katika nchi ali-yozaliwa, yaani, katika Uru wa Wakaldayo. (29) Abram na Nahori wakajitwalia wake. Jina la mkewe Abram aliitwa Sarai, na jina la mkewe Nahori aliitwa Milka, binti Harani, ambaye alikuwa baba wa Milka na wa Iska. (30) Na Sarai alikuwa tasa, hakuwa na mtoto. (31) Tera akamtwa Abram mwanawe, na Lutu mwana wa Harani, mwana wa mwanawe, na Sarai mkewe, mke wa Abram mwanawe, wakatoka wote katika Uru wa Wakaldayo, waende nchi ya Kanaani,

MUNGU ASEMA NA MWANADAMU

wakafika mpaka Harani wakakaa huko.
(32) Siku za Tera zilikuwa miaka mia mbili na mitano; Tera akafa katika Harani.

12:1-9

BWANA akamwambia Abramam, Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha; (2) nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kuli kuza jina lako; nawe uwe baraka; (3) nami nitawabariki wakubarikiyo, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa. (4) Basi Abramam akaenda, kama BWANA alivyomwamuru; Lutu akaenda pamoja naye. Naye Abramam alikuwa mtu wa miaka sabini na mitano alipotoka Harani. (5) Abramam akamchukua Sarai mke we, na Lutu mwana wa nduguye, na vitu vyao vyote walivyokuwa wamejipatia, na hao watu waliowapata huko Harani, wakato ka ili kwenda nchi ya Kanaani; nao wakaingia katika nchi ya Kanaani. (6) Abramam akapita katikati ya nchi mpaka mahali patakatifu pa Shekemu; mpaka mwaloni wa More. Na Wakanaani siku zile walikaa katika nchi hiyo. (7) BWANA akamtokea Abramam, akasema, Uzao wako nitawapa nchi hii. Naye huko akamjengea madhabahu BWANA aliyemtokea. (8) Kisha akaondoka huko akaenda mpaka mlima ulio upande wa mashariki wa Betheli, akaipiga hema yake; alikuwa na Betheli upande wa magharibi, na Ai upande wa mashariki; akamjengea BWANA madhabahu huko, akaliitia jina la BWANA. (9) Naye Abramam akasafiri, akazidi kwenda pande za kusini.

AMU ASIYE NA CHOYO

MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo 13:1-18

Katika masomo yaliyopita tulijifunza juu ya mtu mmoja aliyekuwa mchoyo sana. Mtu huyu aliitwa Kaini. Alikuwa mwana wa mwanamume na mwanamke wa kwanza duniani. Kaini alijaa choyo na wivu nyingi sana hata akamwua nduguye. Walakini katika somo hili la leo, tutajifunza habari za mtu mmoja ambaye hakuwa na choyo hata kidogo. Mtu huyu ndiye yule tuliyejifunza habari zake katika somo lililopita ambaye aliitwa Abram.

Abramu hakukaa Kanaani siku nyingi kwa sababu ya upungufu wa chakula. Ali-mchukua Sarai mkewe wakaenda Misri ambako kulikuwa na chakula kingi. Lakini hata huko Misri Abramu hakukaa siku nyingi. Mungu hakutaka Abramu kukaa Misri, nchi ya watu waliopenda dhambi, kwa hiyo alimpangia kurudi Kanaani.

Wakati Abramu aliporudi Betheli, katika Kanaani, alikuwa tajiri sana. Alikuwa na ng'ombe na fedha na dhahabu nyingi. Alirudi Kanaani akiwa pamoja na Sarai mkewe na Lutu mtoto wa ndugu yake. Wote wawili walikuwa na watumishi wengi.

Wakati Abramu alipokuwa Betheli mbeleni, alijenga madhabahu ambapo ange-mwabudu Mungu. Aliporudi huko, aliliita tena jina la Mungu, akamsujudia. Abramu alikuwako tena katika nchi ambayo Mungu alimtaka kuwa. Na kwa mara nyingine tena Mungu angambariki.

Lutu ambaye alikaa na Abramam ndugu ya baba yake pia alikuwa tajiri. Alikuwa na mifugo mingi. Alikuwa na watumishi wengi. Watumishi hao wa Lutu walijaribu kupata mahali pa kuwalisha kondoo na ng'ombe; na watumishi wa Abramam pia walijaribu kufanya hivyo. Makundi haya mawili walikuwa na hakika kwamba walistahili mahali pema pa kulisha mifugo. Je! unadhani kwamba kulitokea nini kati yao? Ndiyo, walianza kugombana wao kwa wao.



Kumbuka kwamba nchi hii Mungu alimwahidi Abramam. Tena Abramam alikuwa mzee na kiongozi wa jamaa hiyo. Yeye ndiye aliye-stahili kufanya uchaguzi wa kwanza. Labda ikiwa alitaka angalimwambia Lutu, "Nchi hii ni yangu. Ondoka, uende kutafuta mahali pengine pa malisho." Lakini Abramam hakufanya hivyo.

Abramam alitaka kukomesha ugomvi kati ya watumishi wake na watumishi wa Lutu,

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

mtoto wa nduguye. Inaonekana kwamba wangeendelea kugombana kama wangeendelea kukaa pamoja kwa sababu hakukuwa na majani ya kutosha mifugo yao yote. Njia ya pekee ambayo kwayo wangeweza kuwa na amani ilikuwa ni kutengana, yaani, Lutu kwenda upande mmoja na Abram uenda upande mwingine.

Kwa hiyo Abram alimwambia Lutu, "Usiwepo ugomvi kati ya mimi na wewe. Sisi tu ndugu. Ni lazima tukae kwa upendo. Basi chagua upande unaotaka kwenda, nami nitakwenda upande mwingine."

Je! wakati Abram na Lutu waliposimama na kutazama upande wa kuume na wa kushoto waliona nini? Nchi iliyokuwa upande wa kushoto (magharibi) ilikuwa ya milima. Katika nchi kama hiyo ingebidi kondoo na ng'ombe kutafuta majani ya kula kwa muda mrefu. Ingekuwa vigumu sana kuwalisha. Lakini katika upande wa kuume (mashariki) kulikuwa na Bonde la mto Yordani. Kulikuwa na vijito vingi vidogo vidogo vilivyotoka milimani na kuingia katika mto huu, na Bonde lile lote lilifunikwa na majani mabichi. Je! unadhania kuwa ni nchi ipi ambayo ingalimpasa Lutu kuchagua? Kumbuka kwamba Abram alikwisha kukaa na Lutu kwa miaka mingi sana. Alikwisha kumfanyia Lutu mambo mengi. Lakini Lutu alichagua Bonde lile la Yordani lililokuwa na maji mengi. Lutu alikuwa akijifikiria yeye mwenyewe na utajiri wake. Alikuwa mchoyo. Aliwafikiria wanyama wake tu bila kuwafikiria watoto wake. Wakati mwingine kuna vitu fulani ambavyo ni vya umuhimu zaidi kuliko wanyama na utajiri. Bonde lile la Yordani lilikuwa

zuri kwa mifugo ya Lutu, lakini halikuwa zuri kwa watoto wake. Lutu alipiga hema yake karibu na mji wa Sodoma. Katika mji huu wa Sodoma kulikaa watu waovu sana. Je! unafikiri watu hawa walikuwa na mvuto gani kwa watoto wa Lutu? Ndiyo, watoto wa Lutu walipata ugumu wa kukaa karibu na watu hawa waovu na kuendelea kuwa waaminifu kwa Mungu. Lutu alifanya uchaguo wa choyo ambao ulikuwa kosa mbaya sana.

Je! wakati Abramam alipoinua macho yake na kutazama nchi baada ya Lutu kufanya uchaguo wake, unadhani alifikiria nini? Mungu alisema na Abramam tena. Ali-mwambia Abramam ya kwamba nchi yote ambayo aliweza kuona kutoka mahali pale alipokuwa ingekuwa yake na ya watoto wake. Taifa lake lenye nguvu lingekaa katika nchi hiyo. Mungu alikwisha kumwahidi Abramam hii zamani, na sasa aliirudia tena kwa Abramam. Ahadi hiyo ya Mungu kwa Abramam ilitimia kama sikuzote. Jamaa ya Abramam waliongezeka wakawa taifa kubwa la watu, wakakaa katika nchi hiyo.

KAZI YA KUFANYA:

Jaza nafasi zilizoachwa kwa maneno ya kweli.

Abramam hakukaa Kanaani kwa sababu ya upungufu wa _____.

Alikwenda _____ ambako alikaa siku chache.

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

Kutoka huko, Mungu alimwongoza Abramam
kurudi katika nchi aliyokwisha kumpa
iliyoitwa _____.

Wakati Abramam alipokuwa katika nchi
hiyo zamani, alijenga _____
ya kumwabudu Mungu.

Andika herufi "K" kando ya sentensi
ya kweli, na uandike herufi "M" kando ya
sentensi ambazo si kweli.

_____ Abramam alimwabudu Mungu mahali po-
pote alipokwenda.

_____ Wachungaji wa Lutu walianza kugo-
mbana na wachungaji wa Abramam.

_____ Wachungaji wale hawakulipwa msha-
hara wa kutosha.

_____ Nchi ile ilikuwa ndogo sana kwa
wachungaji wa Lutu na wa Abramam.

_____ Wachungaji wa Abramam walikuwa
wakiiba kondoo nyingine za Lutu.

Andika kwa maneno yako mwenyewe
mambo ambayo Abramam alimwambia Lutu kufa-
nya.



AMU ASIYE NA CHOYO

Lutu alichagua Bonde zuri la Yordani lenye maji mengi. Majani mabichi yaliyo-kuwa katika Bonde hilo yangekuwa malisho mema kwa mifugo yake. Chora mviringo kwa maneno ya kweli juu ya Lutu. Upige mstari chini ya maneno yale yanayoeleza habari za Abramamu.

Mwema

Asiye mchoyo

Mchoyo

Mcha Mungu

Asiyefikiri

Tafuta mahali ambapo Lutu alikwenda baada ya kujitenga na Abramamu, amu wake. Tazama Mwanzo 13:12-13.

Je! kisha Abramamu alikaa katika nchi gani _____

Je! Lutu alikaa wapi? _____

Lutu alipiga hema yake karibu na mji gani? _____

Je! ni watu wa namna gani waliokaa katika mji huo? _____

Endelea kusoma vifungu hivyo vya Biblia, kisha uone mambo ambayo Mungu alimwambia Abramamu. Halafu kata maneno yote yasiyo kweli ambayo yako katika alama hii ().

Inua macho yako utazame upande wa (Sodoma) (kaskazini, kusini, mashariki na magharibi). (Sehemu) (Nchi hii yote) unayoiona itakuwa yako na uzao wako hata milele.

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

Na uzao wako nitaufanya uwe kama
(mavumbi) (miamba) ya nchi.

Mungu alikuwa na maana kwamba uzao wa
Abramu haungeweza kuhesabiwa (Tembea)
(Safiri kwa motakaa) katika nchi hii,
maana nitakupa wewe.

Mungu aliahidi kumbariki Abramu kwa
kumpa uzao mwingi na nchi kubwa.
Abramu alitaka kumshukuru Mungu.
Alijenga_____.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

*"Kwa pendo la udugu, mpendane ninyi
kwa ninyi; kwa heshima mkiwatangulia
wenzenu."*
Warumi 12:10

Je! mtu gani katika somo hili la
leo ambaye alikuwa mchoyo? _____

Je! mtu gani ambaye hakuwa mchoyo?

Kifungu chako cha kukumbuka kinakwa-
mbia usiwe mchoyo, kuwa mwema. Maana yake
ni kwamba, unapaswa kuwafikiria wengine
kabla ya kujifikiria wewe mwenyewe. Je!
unaweza kufanya hivyo kwa jinsi gani?

MANENO YA KUJIFUNZA:

amu.....ndugu mwanamume wa baba.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Mwanzo 13:1-18

Abramu akapanda kutoka Misri , yeye na mkewe, na kila alichokuwa nacho, na Lutu pamoja naye, mpaka kusini. (2) Naye Abramu alikuwa ni tajiri sana kwa mifugo, kwa fedha, na kwa dhahabu. (3) Akaendelea kusafiri kutoka kusini mpaka Betheli, mahali pale palipokuwapo hema yake kwanza kati ya Betheli na Ai; (4) napo ndipo palipokuwa na madhabahu aliyofanya hapo kwanza; naye Abramu akaliitia jina la BWANA hapo. (5) Na Lutu aliyesafiri pamoja na Abramu, yeye naye alikuwa na maku-ndi ya ng'ombe na kondoo, na hema. (6) Na ile nchi haikuwatosha, ili wakae pamoja; maana mali zao zilikuwa nyingi, hata wasiweze kukaa pamoja. (7) Kukawako ugomvi kati ya wachunga wanyama wa Abramu, na wachunga wanyama wa Lutu; na siku zile Wakanaani na Waperizi walikuwa wakika katika nchi. (8) Abramu akamwambia Lutu, Basi, usiwepo ugomvi, nakusihi, kati ya mimi na wewe, wala kati ya wachungaji wangu na wachungaji wako; maana sisi tu ndugu. (9) Je! nchi hii yote haiko mbele yako? basi ujitenge nami, nakusihi; ukienda upande wa kushoto, nita-
kwenda upande wa kuume; ukienda upande wa kuume, nitakwenda upande wa kushoto. (10) Lutu akainua macho yake, akaliona Bonde lote la Yordani, ya kwamba lote pia lina maji, kabla BWANA hajaharibu Sodoma na Gomora, lilikuwa kama bustani ya BWANA, kama nchi ya Misri hapo unapokwenda Soari. (11) Basi Lutu akajichagulia Bonde lote la Yordani; Lutu akasafiri kwenda upande wa mashariki; wakatengana

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

wao kwa wao. (12) Abramam akakaa katika nchi ya Kanaan, na Lutu akakaa katika miji ya lile Bonde; akajongeza hema yake mpaka Sodoma. (13) Lakini watu wa Sodoma walikuwa wabaya, wenye kufanya dhambi nyingi sana juu ya BWANA.

(14) BWANA akamwambia Abramam, alipokwisha kutengana na Lutu, Inua sasa macho yako, ukatazame kutoka hapo ulipo, upande wa kaskazini, na wa kusini na wa mashariki na wa magharibi; (15) maana nchi hii yote uionayo, nitakupa wewe na uzao wako hata milele. (16) Na uzao wako nitaufanya uwe kama mavumbi ya nchi; hata mtu akiweza kuyahesabu mavumbi ya nchi, na uzao wako nao utahesabika. (17) Ondoka, ukatembee katika nchi hii, katika mapana yake, na marefu yake, maana nitakupa wewe nchi hiyo. (18) Basi Abramam akajongeza hema yake, akaja akakaa kwenye mialoni ya Mamre, nayo ni miti iliyoko Hebroni, akamjengea BWANA madhabahu huko.

MUNGU HUSHIRIKI SIRI FULANI

MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo 15:1,5,18;
17:1-8, 15-19

Je! unajua jambo lililompata Lutu baada ya kuhamia Sodoma, mji uliokuwa umejaa maovu? Mji huu wa Sodoma na miji mingine minne katika tambarare ya Yordani, kila mmoja ulikuwa na mfalme wake, lakini wafalme hawa watano waliotawala miji hiyo walitawaliwa na mfalme mmoja aliye-kuwa na mamlaka kushinda wao. Siku moja, wafalme hawa watano walikata shauri kumwasi mfalme yule aliyewatawala. Katika vita iliyotokea, wafalme wa Sodoma na Gomora walishindwa, na miji yao ilisha-mbuliwa, na mali yao yote ikatwaliwa. Lutu na mkewe walikamatwa mateka kwa sababu walikaa katika mji huo wa Sodoma.

Habari zilipomfikia Abramu katika makao yake, aliwapa silaha watumishi wake 318, akawashambulia maadui usiku. Alimwoko Lutu pamoja na watu wote wa Sodoma. Abramu alikuwa mtu aliyependa amani, lakini tena alikuwa na ushujaa wa kutumia wakati ulipokuwa ni muhimu kufanya hivyo.

Kwa sababu ya ushujaa huo wa Abramu, mfalme wa Sodoma alitaka kumtuza vitu vyote ambavyo viliibiwa kutoka Sodoma. Lakini Abramu alimwambia mtawala huyu mwovu ya kwamba hangechukua tuzo lo lote. Hakutaka mfalme huyo wa Sodoma kudai ya kwamba alimtajirisha. Utajiri wake (Abramu) ulikuwa umetoka kwa Mungu, na alitaka kubaki mwaminifu kwa Mungu. Baraka ya Mwenyezi Mungu ni nzuri kuliko

zawadi ya mfalme ye yote.

Wakati Abramam aliporejea nyumbani kutoka vitani, alichoka. Bila shaka palikuwa na woga moyoni mwake kwa sababu Mungu alisema naye, akamwambia, "Usiogope." Pia, Mungu alimwambia Abramam ya kwamba angekuwa ngao yake. Maana yake ni kwamba Mungu angesimama katikati ya Abramam na maadui zake, na kumlinda. Kisha Mungu alimwambia Abramam ya kwamba angekuwa kitu kingine chenye thamani zaidi kuliko ngao kwake. Alimwambia ya kwamba angekuwa "thawabu yake kubwa sana." Thawabu hii ilikuwa kubwa zaidi kuliko tuzo lo lote ambalo Abramam angalipokea kutoka kwa mfalme ye yote.

Roho ya Abramam ilikuwa bado ina wasiwasi. Kwa hiyo aliuliza, "Ee Bwana Mungu, utanipa nini, nami naenda zangu hali sina mtoto?" Abramam alitazamia kupata mtoto ambaye Mungu aliahidi kumpa kwa muda wa miaka kumi, lakini bado hakupata. Alitaka sana mtoto mume kuliko kitu cho chote ulimwenguni. Hakuwa hata na mtu ambaye angerithi utajiri wake, kwa hiyo ingekuwa muhimu sana kwake kama angepata mrithi wake.

Ilikuwa desturi siku zile kwa mtu asiye na mwana kumchagua mkuu wa watumishi wake kurithi utajiri wake na kusimamia jamaa yake baada ya yeye kufa. Lakini Mungu alisema na Abramam tena, akamwahidi ya kwamba mtumishi wake hangekuwa mrithi wake. Ili kumfanya Abramam kuamini ahadi hii, Mungu alimtoa Abramam nje usiku,

akamwonyesha nyota. Nyota hizo zilikuwa nyingi sana zisizoweza kuhesabiwa. Mungu alimwambia Abramam ya kwamba uzao wake ungekuwa kama nyota hizo. Abramam akamwamini Bwana.



Pia, Mungu alimwambia Abramam ya kwamba alimtoa Uru ili kumpa nchi hiyo aliyekuwa akikaa sasa.

Lakini zaidi ya miaka 13 au 14 zilipita, na Abramam na Sarai walikuwa bado kupata mtoto. Je! Mungu alikuwa amesahau ahadi yake kwao? Abramam alikuwa mtu wa miaka sabini na mitano wakati Mungu alipomwahidi kumpatia mwana. Sasa alikuwa mtu wa miaka tisini na tisa Mungu alimjia Abramam kwa mara nyingine tena. Wakati Abramam alipomsikia Mungu akisema naye, alianguka kifudifudi. Hii ilikuwa njia yake ya kuonyesha heshima kwa Mungu, kama tunavyoinamisha vichwa vyetu kuomba. Mungu alisema tena ahadi

ile yake kwa Abramumu, na kila wakati alipozungumza juu ya ahadi hiyo, aliongeza jambo fulani kwake. Wakati huu alisema Abramumu angekuwa baba wa mataifa mengi, na kwamba wafalme wangepata katika uzao wake. Bila shaka jambo hili lilikuwa gumu sana kwa Abramumu kuliadini kwa sababu mpaka sasa walikuwa hawajapata mtoto kama Mungu alivyowaahidi. Iliwasaidia waweze kuadini, Mungu alimpa Abramumu jina jipya. Kuanzia wakati huo jina lake lingekuwa Ibrahimumu, maana yake, "baba wa mataifa mengi."

Pia, Mungu alimpa Sarafi jina jipya. Kuanzia wakati huo angeitwa Sara, maana yake "binti mfalme." Ibrahimumu alifurahia sana jambo hili hata akacheke. Moyo wake ulijaa furaha wakati alipofikiria kupata mwana wake mwenyewe.

Kisha Mungu alimwambia Ibrahimumu ya kwamba watamwita mwana wao Isaka, jina ambalo maana yake ni "kicheko." Ibrahimumu na Sara walifurahi sana kwa sababu baada ya siku chache tu wangepata mtoto wa kurithi ahadi zote za Mungu za ajabu ambazo Mungu aliwaahidi. Hawakufikiria utajiri wao wa ng'ombe na kondoo. Utajiri wao hasa ulikuwa katika ahadi ambazo Mungu aliwaahidi.

Baada ya muda kupita, kama Mungu alivyoahidi, Sara alimzalia Ibrahimumu mwana. Kwa vile ilikuwa desturi yao kumtii Mungu, walimwita mwana huyo Isaka kwa sababu Mungu aliwaambia kufanya hivyo. Walifurahi na kumshukuru Mungu sana.

KAZI YA KUFANYA:

Katika Mwanzo 15:1, 5, na 18 tunasoma juu ya ahadi tatu ambazo Mungu aliagana na Abram. Chora mistari kutoka kwa neno AHADI mpaka kwa ahadi zile tatu za Mungu.

Mimi ni Ngao yako na
thawabu yako kubwa sana.

Nitakupigania vita.

Nitakutajirisha sana.

AHADI

Uzao wako utakuwa mwingi kama nyota.

Uzao wako nitawapa nchi
ilie iliyo katikati ya
mito miwili.

Mungu alimwahidi Ibrahimu ya kwamba uzao wake ungekuwa mwingi. Je! Mungu alisema ya kwamba uzao huo wa Ibrahimu ungekuwa kama nini zisizoweza kuhesabiwa?

Abramu alimpenda Bwana kweli na kumwamini. Yeye na Bwana walikuwa marafiki wema. Mungu alisema naye tena. Soma Mwanzo 17:1-2

Je! Abramu alikuwa mtu wa miaka mingapi wakati huu? _____

Je! Mungu alijiitaje mwenyewe?

Je! Bwana alimwambia Abramam kufanya nini?

Bwana alimwahidi Abramam tena ya kamba angempa uzao mwingi. Mungu aligeuza jina la Abramam. Tafuta ya kuwa jina la Abramam jipya liliitwaje. Andika namba ya kifungu cha kweli cha Biblia kando ya kila sentensi zifuatazo. (Tazama Mwanzo 17:3-5)

— Mungu alifanya agano (ahadi) lake na Abramam.

— Wakati Mungu alipoanza kusema, Abramam alianguka kifudifudi konyesha heshima na upendo wake kwake.

— Mungu aligeuza jina Abramam kuwa Ibrahimu.

— Jina Ibrahimu maana yake ni "baba wa mataifa mengi."

Hapa kuna ahadi nyingine za ajabu ambazo Mungu alimwahidi Ibrahimu. Andika herufi hii "X" kwenye mstari ulio kando ya kila sentensi ya kweli. Vifungu 6-8 vitakusaidia.

— Nitakufanya kuwa mataifa.

— Mataifa yatatoka kwa watoto wa watumishi wako.

— Wafalme watatoka kwako.

MUNGU HUSHIRIKI SIRI FULANI

— Nitakuwa Mungu kwako na kwa uzao wako (Waisraeli).

— Nitafanya ahadi yangu nawe kwa miaka 50.

— Nitakupa wewe na uzao wako sehemu ndogo ya nchi ya Kanaani.

Pia, Mungu alimpa mkewe Ibrahimu jina jipya. Tafuta jina hilo na maana yake. Soma vifungu 15-16.

Jina la kwanza la mkewe Ibrahimu liliitwaje? _____

Jina lake jipya liliitwaje? _____

Mungu aliahidi kumpa Sara kitu gani ambacho alikuwa amekwisha kuahidi kumpa Ibrahimu? _____

Kwa vile Ibrahimu angekuwa baba wa mataifa mengi, Sara angekuwa _____ wa _____.

Ibrahimu na Sara walifurahi sana wali-posikia habari hii.

Je! Mungu aliwaambia kumwita mtoto wa kwanza jina gani? _____

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye alitwa rafiki wa Mungu." Y. Yobo 2:23

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

Uaminifu katika Mungu ni Imani.
Katika Yohana 10:9 ulijifunza ya kwamba
Yesu mwenyewe ndiye mlango mbinguni.
Ikiwa una imani, basi unaamini kwamba
Yesu anakuokoa katika dhambi. Una ufu-
nguo wa kuingia mbinguni. Kama huna imani,
umefungiwa nje ya mbinguni, na nje ya
baraka nyingine nyingi. Mwombe Mungu
kukupa ufunguo huu sasa.



MANENO YA KUJIFUNZA:

uzao.....kilichozaliwa, namna ya
kuzalikana
ngao.....kitu bapa kilichotengene-
zwa kwa ngozi ya mnyama
au mti cha kuingia mishale
au silaha za adui.
mrithi.....mtu arithiye, apataye kwa
haki mali iliyoachwa na
mtu aliyekufa.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Mwanzo 15:1, 5, 18, 17:1-8, 15-19

Baada ya mambo hayo neno la BWANA
likamjia Abram katika njozi, likinena,
Usiogope, Abram, Mimi ni ngao yako, na
thawabu yako kubwa sana.

MUNGU HUSHIRIKI SIRI FULANI

(5) Akamleta nje, akasema, Tazama sasa mbinguni, kazihesabu nyota, kama ukiweza kuzihesabu. Akamwambia, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako.

(18) Siku ile BWANA akafanya agano na Abramamu, akasema, Uzao wako nimewapa nchi hii, kutoka mto wa Misri mpaka huo mto mkubwa, mto Frati.

17:1-8

Abramu alipokuwa mtu wa miaka tisini na kenda, BWANA akamtokea Abramamu, akamwambia, Mimi ni Mungu Mwenyezi, uende mbele yangu, ukawe mkamilifu. (2) Nami nitafanya agano langu kati ya mimi na wewe, nami nitakuzidisha sana sana. (3) Abramamu akaanguka kifudufudi. Mungu akamwambia, akasema, (4) Mimi, agano langu nimefanya nawe, nawe utakuwa baba wa mataifa mengi, (5) wala jina lako hutaitwa tena Abramamu, lakini jina lako litakuwa Ibrahimu, kwani nimekuweka uwe baba wa mataifa mengi. (6) Nitakufanya uwe na uzao mwingi sana, nami nitakufanya kuwa mataifa, na wafalme watatoka kwako. (7) Agano langu nitalifanya imara kati ya mimi na wewe, na uzao wako baada yako, na vizazi vyao, kuwa agano la milele, kwamba nitakuwa Mungu kwako na kwa uzao wako baada yako. (8) Nami nitakupua wewe na uzao wako baada yako nchi hii unayoikaa ugeni, nchi yote ya Kanaani, kuwa milki ya milele; nami nitakuwa Mungu wao.

15-19

Mungu akamwambia Ibrahimu, Sarai mkeo, hutamwita jina lake Sarai, kwa kuwa jina lake litakuwa Sara. (16) Nami nita-

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

mbariki, na tena nitakupa mwana kwake, naam, nitambariki, naye atakuwa mama wa mataifa, na wafalme wa kabila za watu watatoka kwake. (17) Ndipo Ibrahimu akaanguka kifudifudi akachekeka, akasema moyoni, Je! Mtu wa umri wa miaka mia, kwake atazaliwa mtoto? Naye Sara mwenye umri wa miaka tisini atazaa? (18) Ibrahimu akamwambia Mungu, Lau kwamba Ishmaeli angeishi mbele yako. (19) Mungu akasema, Sivyo, lakini Sara mkeo atakuzalia mwana wa kiume, nawe utamwita jina lake Isaka. Nami nitafanya agano langu imara kwake kuwa agano la milele kwa ajili ya uzao wake baada yake.

MUNGU ASHUGHULIKA NA WATEULE WAKE

MASOMO YA BIBLIA: YOSHUA 1:1-9

Ibrahimu alingojea kwa miaka ishiri-ni na mitano kwa Mungu kutimiza ahadi yake kwake. Alimwamini Mungu na alijua kwamba angetimiza ahadi yake. Tunaweza kufahamu sababu iliyomfanya Ibrahimu kusi-fiwa kwa imani yake.

Isaka, mwanawe Ibrahimu alikua, na baada ya miaka fulani kupita, akawa baba ya watoto ambao pia walizaa watoto wao. Uzao mwingi wa Ibrahimu walisikia habari juu ya ahadi ya Mungu kwamba angewafanya kuwa taifa, na kwamba wangekaa katika nchi ile ya Kanaani. Wengine walimwamini Mungu daima, wakabarikiwa. Wengine wali-chagua kuishi katika njia zao wenyewe za uovu, na waliadhibiwa daima.

Dhambi ilikuwa na mvuto mkubwa mai-shani mwa watu wengi, na kwa ajili hiyo watu waliadhibiwa. Watu ambao Mungu ali-wachagua kuwa watu wake, sikuzote hawaku-kaa katika nchi ambayo Mungu aliwapa. Hata mwishoe walikwenda Misri kutafuta chakula wakati njaa kubwa ilipotokea katika nchi yao. Katika Misri idadi ya Waebrania iliongezeka sana mpaka Wamisri wakaogopa. Waliogopa kwa sababu Waebrania walikuwa wengi sana hata kama wangependa kupigana vita nao wangeweza kuwashinda. Kwa hiyo Wamisri waliwatesa sana watu hawa wa Mungu. Waliwalazimisha kufanya kazi kama watumwa, na kazi yao ilikuwa ngumu sana. Baada ya muda fulani, Mungu

alimchagua mtu mmoja kuwaongoza watu hawa wake kutoka katika nchi hii ya utumwa na kuingia katika nchi aliyoahidi kuwapa. Mtu huyu alikuwa Musa, na aliwaongoza watu wa Mungu kutoka katika utumwa.

Dhambi ilikuwa bado ina mvuto, lakini wale waliokuwa waaminifu kwa Mungu walituzwa. Mara nyingi watu walikufa moyo na kuwa na shaka juu ya Mungu. Walikuwa wamekwisha kutangatanga jangwani kwa miaka arobaini kwa sababu ya dhambi zao. Hatimaye Mungu alimpa Musa sheria zake ili watu wangeweza kujua mambo aliyowataka kufanya. Lakini mpaka sasa hawakufanya mapenzi ya Mungu. Sheria hizi zilitwa Amri Kumi.

Mwishoe dhambi ilizidi kuongezeka sana hata Mungu akasema ni lazima watu wake kutangatanga jangwani mpaka wakati ambapo wazee wote wangekufa, na watoto wao kukua na kuwa kizazi kipya. Wazee waliokuwa na shaka juu ya Mungu na wale waliomtenda Mungu dhambi mara kwa mara, Mungu alisema hawangeweza kuingia katika nchi ya ahadi. Na wakati ambapo kizazi hicho kipya kingekuwa na watu wazima, ndipo Mungu angewaongoza kuingia katika nchi ile aliyoahidi kuwapa miaka mingi sana iliyopita. Kiongozi mpya ambaye Mungu alimchagua kuwaingiza watu wake katika nchi yao ya ahadi aliitwa Yoshua.

Mungu alisema na mwanadamu kwa mara nyingine. Aliahidi Yoshua, baada ya kumwita kumfanyia kazi maalum. Katika Yoshua



1:3 Mungu alifanya mara ya pili ahadi yake juu ya nchi ile ambayo watu wake wangekaa. Alise- ma kila mahali ambapo wangeka- nyaga angempa Yoshua. Pia Mungu aliahidi kuwa pamoja na Yoshua kama alivyokuwa pamo- ja na Musa ali- yemtangulia.

Alimtia Yoshua moyo kuwa hodari na kuwa na ushujaa kwa sababu angemtumia kutimiza ahadi aliyowaahidi watu wake miaka mingi iliyopita. Alimtia Yoshua moyo kuwa mwan- galifu sana kufanya mambo yote ambayo iliamriwa na sheria ya Musa. Alimwambia kufikiria sheria yake mchana na usiku na kutia juhudi zake zote katika kutenda sawasawa Sheria ya Mungu. Mungu alimwa- mbia Yoshua kwamba, kama angefanya hivyo, basi hangepaswa kuwa na woga wo wote wala hofu kwa sababu angekuwa pamoja naye mahali po pote aendapo.

Katika miezi na miaka iliyofuata, Yoshua alijaribu kufanya kama alivyofundi- shwa. Kulikuwa na siku nyingine za mata- tizo na taabu, lakini Yoshua aliwaongoza watu kuamini kwamba Mungu angetimiza aha- di zake kwao. Wengine kati ya watu wale walikuwa na imani, na wengine walikuwa na shaka. Mwishoe, Yoshua alisema nao

wazi. Aliwaambia ya kwamba Mungu aliwaleta katika nchi ambayo walikuwa hawajapata kuiona kamwe, na kwamba ingekuwa yao. Wangukuwa na miji ambayo hawakuje-nga, na chakula ambacho hawakupanda. Mungu aliwabariki katika njia hiyo ili kutimiza ahadi yake kwa Ibrahimu na kwa wale wanaomfuata. Kisha Yoshua aliwauliza watu wale ya kwamba wanguchagua kufanya nini. Aliwauliza kama wanguchagua kutumikia miungu wa babu zao, au kutumikia tamaa zao wenyewe, au kumtumikia Mungu mmoja wa kweli aliye hai. Kila mmoja wao alipaswa kuchagua yeye mwenyewe kama angemtumikia nani, lakini Yoshua alisema yeye pamoja na nyumba yake wanguemtumikia Mungu. Kisha watu wale walimwambia Yoshua, "Bwana, Mungu wetu, ndiye tutakayemtumikia; na sauti yake ndiyo tutakayo-itii." (Yoshua 24:24)

Watu wale hatimaye walitambua kwamba Mungu alikuwa mwaminifu kwao, na kwamba alitimiza ahadi zake kwao. Walijua kwamba iliwapasa kumtumikia Mungu kwa ajili hiyo.

KAZI YA KUFANYA:

Mungu alimwahidi Ibrahimu ya kwamba uzao wake ungekuwa mwingi. Siku ya leo tumejifunza kwamba Mungu alitimiza ahadi hiyo kama anavyotimiza ahadi zake siku-zote. Jaza nafasi zilizoachwa kuonyesha jinsi Mungu anavyoshughulika na watu wake.

MUNGU ASHUGHULIKA NA WATEULE WAKE

Watu wengine, daima walimwamini Mungu, na Mungu_____.

Wengine walichagua kuishi katika njia zao wenyewe za uovu, na Mungu_____ daima.

Taja majina ya watu watatu ambao Mungu alisema nao na kuagana nao.

Mungu aliwapa watu sheria za kufuata ili wangeweza kujua jambo walilotazamiwa kufanya. Musa aliandika sheria hizo kama Mungu alivyomwambia. Sheria hizo ziliitwa

_____ .

Lakini watu waliendelea kutenda dhambi. Andika herufi "M" kando ya sentensi ambazo si kweli.

— Mungu alitimiza ahadi yake kwamba uzao wa Ibrahimu ungekuwa mwingi.

— Watu wote wa Mungu walimwamini na kufanya mambo aliyowaambia.

— Mungu aliwaadhibu watu waliotenda dhambi kwa kufanya mimea yao kuto-
kua.

— Watu wa Mungu walitangatanga jangwani kwa miaka 40 kwa sababu ya dhambi zao.

— Mungu hakuwaruhusu watu wake wengine kuingia katika Nchi ya Ahadi kwa sababu ya dhambi zao.

— Mungu alimwita Yoshua, hasa kuwa-ingiza watu wake katika nchi yao.

Wakati Mungu alipomwita Yoshua alisema ahadi yake tena kwake. Je! Mungu alisema angempa Yoshua nchi ile kiasi gani?

Je! ni ahadi ipi nyingine ambayo Mungu alimwahidi Yoshua katika Yoshua 1:5?

Je! Mungu alimwambia Yoshua kufanya nini? Chora mviringo kwa jibu lililo sawa.

Kuwa hodari na shujaa.

Usitoke nje usiku.

Jihadhari uwaonapo maadui.

Tenda sawasawa sheria yote aliyoku-amuru Musa.

Kuwa na mlinzi wako wakati wote.

Usiogope.

Usife moyo.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Bwana, Mungu wetu, ndiye tutakaye-
mtumikia; na sauti yake ndiyo tuta-
kayoitii." Yoshua 24:24

Yoshua alimsikia Mungu akisema naye, akamtii. Lakini watu wake wengi waliendelea kutenda dhambi. Alitaka kuwaongoza katika njia ya Mungu, lakini kila mmoja alipaswa kuchagua kama alitaka kufuata njia hiyo au la. Hivyo ndivyo ilivyo sasa. Kila mmoja wetu ni lazima kuchagua njia ya kuishi. Wazazi wanaomcha Mungu, wachungaji, waalimu, wote wanataka kutusaidia, lakini ni lazima kujikatia shauri sisi wenyewe. Yoshua aliwaambia watu wake kumchagua yule ambaye walitaka kumtumikia. Wewe pia ni lazima kuchagua. Chora mstari hadi kwa njia unayotaka kufuata katika maisha yako.

JE! NITAMTUMIKIA NANI?

MIUNGU WA
UWONGO

MUNGU MMOJA
WA KWELI NA
ALIYE HAI

TAMAA
ZANGU ZA
UCHOYO



KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

MANENO YA KUJIFUNZA:

kanyaga.....kuvyoga, kugandamiza
kwa miguu.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Yoshua 1:1-9

Ikawa baada ya kufa kwake Musa, mtumishi wa BWANA, BWANA akamwambia Yoshua mwana wa Nuni, mtumishi wa Musa, akasema, (2) Musa mtumishi wangu amekufa; haya basi, ondoka, vuka mto huu wa Yordani; wewe na watu hawa wote, mkaende hata nchi niwapayo wana wa Israeli. (3) Kila mahali zitakapopakanyaga nyayo za miguu yenu, nimewapa ninyi, kama nilivyomwambia Musa. (4) Tangu jangwa hili na mlima huu, Lebanoni, mpaka mto ule mkubwa, mto wa Frati, nchi yote ya Wahiti, tena mpaka bahari ile kubwa upande wa machweo ya jua, hapo ndipo patakapokuwa mpaka wenu. (5) Hapatakuwa mtu ye yote atakayeweza kusimama mbele yako siku zote za maisha yako; kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe sitakupungukia wala sitakuacha. (6) Uwe hodari na moyo wa ushujaa, maana ni wewe utakayewarithisha watu hawa nchi hii niliyowaapia baba zao ya kwamba nitawapa. (7) Uwe hodari tu na ushujaa mwingi, uangalie kutenda sawasawa na sheria yote aliyokuamuru Musa mtumishi wangu; usiiche, kwenda mkono wa kuume, au wa kushoto, upate kufanikiwa sana kila uendako. (8) Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda

MUNGU ASHUGHULIKA NA WATEULE WAKE

sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa humo; maana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana.

(9) Je! si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa BWANA, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendako.

AHADI KUU YA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Isaya 9:2-7

Mungu aliwalinda watu wake kwa njia ya ajabu wakati alipowatoa katika nchi ambako walitumikia kama watumwa na kuwapeleka katika nchi aliyowaahidi. Mungu alitimiza ahadi hii yake aliyowaahidi miaka mingi sana iliyopita. Mungu hutimiza kila ahadi yake daima.

Mungu aliumba ulimwengu na watu waliomo ndani ili angeweza kuwa na ushirika na mwanadamu ambaye alimwumba kwa mfano wake. Mungu alikusudia ulimwengu kuwa na amani na furaha. Lakini dhambi iliingia ulimwenguni. Mwanadamu, kwa sababu Mungu alimpa uwezo wa kuchagua jambo apendalo, aliamua kujitumikia mwenyewe badala ya kumtumikia Mungu. Kwa hivyo dhambi ilivunja ushirika mwema ambao ulipaswa kuwapo kati ya Mungu na mwanadamu.

Kwa sababu ya dhambi, Mungu alimpa mwanadamu ahadi ya ajabu. Alisema ya kwamba siku moja angemtuma Mwokozi ulimwenguni kuondoa dhambi ya mwanadamu, ili mwanadamu angeweza tena kuwa na ushirika halisi na Mungu. Mwokozi huyu angekuwa Mwana wa Mungu kwa sababu yeye pekee ndiye hakuwa na dhambi, na kwa hiyo angeweza kulipa deni la dhambi ya mwanadamu.

Ahadi ya Mungu ya kumtuma Mwokozi ilisemwa kwa mwanadamu mara nyingi sana. Jinsi Ibrahimu, Isaka, Musa, na Yoshua walimsikia Mungu akiwaahidi ya kwamba

AHADI KUU YA MUNGU

Ndiyo, Mungu aliahidi kutuma Mwokozi ulimwenguni ili kurudisha ushirika ulio-kuwa kati yake na mwanadamu. Mungu alituta-ka sisi kujua mambo mengi juu yake, kwa hiyo alimpa Isaya nabii wake neno lenye mfano wa Masihi aliyeahidiwa kuja. Andika majina manne ambayo Mungu alimpa Mwokozi na ambayo unaweza kupata katika Isaya 9:6.

Andika jibu la kweli katika mstari, ulio kando ya kila swali.

Je! ni jina lipi linalotwambia kwamba Mwokozi angekuwa hekima kuu?

Je! ni jina lipi linalosema kwamba ataishi milele? _____


Je! ni jina lipi linalotwambia kwamba atakomesha chuki, dhambi, na vita?

Je! ni jina lipi linalotufahamisha kwamba ana nguvu zote kwa sababu yeye ni Mungu? _____

Yesu, Mwana wa Mungu, alikuja kutimiza ahadi hizi zote. Andika jina lake katika kisanduku hicho cha katikati

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

kuonyesha jinsi anavyowaunganisha Mungu na mwanadamu kwa mara nyingine.



KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; naye ataitwa jina lake, Mshauri wa Ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa Milele, Mfalme wa Amani."

Isaya 9:6

Mungu alitaka sana kutusamehe dhambi zetu hata akamtoa Mwanawe pekee kufa msalabani kwa ajili yetu. Amekwisha kutimiza wajibu wake. Je! umekwisha kumpokea Mwanawe kama Mwokozi wako ili uweze kusamehewa dhambi zako?

Je! ikiwa bado, utampokea sasa?

MANENO YA KUJIFUNZA:

mnyororo.....vitanzi vya chuma vili-vyongana kufanya mapi-ngu ya kufungia wafu-ngwa.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Isaya 9:2-7

Watu wale waliokwenda katika giza Wameona nuru kuu; Wale waliokaa katika nchi ya uvuli wa mauti, Nuru imewaangaza.

(3) Umeliongeza taifa, umezidisha furaha yao; Wanafurahi mbele zako, Kama furaha ya wakati wa mavuno, Kama watu wafurahi-vyo wagawanyapo nyara. (4) Kwa maana umeivunja nira ya mzigo wake, na gongo la bega lake, na fimbo yake yeye aliye-mwonea, kama katika siku ya Midiani.

(5) Maana silaha zote za mtu mwenye silaha wakati wa mshindo, na mavazi yaliyofingirishwa katika damu, yatakuwa tayari kute-ketezwa, yatakuwa kuni za kutiwa motoni.

(6) Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume; Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani. (7) Maongeo ya enzi yake na amani Hayatakuwa na mwisho kamwe, Katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; Kuuthibitisha na kuutegemeza Kwa hukumu na kwa haki, Tangu sasa na hata milele. Wivu wa BWANA wa majeshi ndio utakaotenda hayo.

KIPAWA KIKUU CHA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Luka 2:1-20, 29-33,
36-39

Mungu alitoa ahadi yake kwa Hawa ambaye hakuwa na furaha katika Bustani ya Edeni. Mungu alisema ya kwamba siku moja, Mtoto wa ajabu angezaliwa. Mtoto huyo angekuwa Mwana wa Mungu ambaye angeangamiza nguvu za Shetani.

Miaka mingi baadaye, Mungu alimwahidi Ibrahimu ya kwamba katika uzao wake mtoto angezaliwa, na mtoto huyo angewabariki watu wote duniani. Wakati unaposoma hadithi juu ya Krismasi, ona jinsi Mungu alivyotimiza ahadi zake kwa Hawa, kwa Ibrahimu, na kwa wengine.

Kaisari Augusto, mfalme wa Kirumi aliamuru kuandikwa orodha ya majina ya wote ili ushuru ungeweza kukusanywa kuto-ka kwa watu wote. Ilikuwa ni lazima kwa kila mtu kuandikwa mjini kwao. Kwa hiyo Yusufu ambaye alikuwa ni wa mbari na jamaa ya Daudi, alikwenda pamoja na Mariamu mkewe Bethlehemu, mji wa Daudi, kuandikwa huko.

Lakini mji huo wa Bethlehemu ulijaa watu wengi sana hata hawakuweza kupata mahali pa kukaa. Mwishoe walipata mahali pa kulala katika zizi. Usiku ule Mariamu alimzaa mwanawe, akamlaza katika hori ya kulia ng'ombe.



Katika nchi ile wali-
kuwako wachungaji wakikaa
makondeni wakiwalinda
kondoo zao. Malaika wa
Mungu aliwatokea kwa ghafu-
la, utukufu wa Mungu ukawa-
ng'aria pande zote. Wali-
ogopa sana.

Malaika alianza kuse-
ma: "Msilogope; kwa kuwa
mimi ninawaletea habari
njema ya furaha kuu itaka-
yokuwa kwa watu wote; maana

leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa
ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana.
Na hii ndiyo ishara kwenu; mtamkuta mtoto
mchanga amevikwa nguo za kitoto, amelala
katika hori ya kulia ng'ombe." (Luka
2:10-12)

Mara walikuwapo pamoja na huyo mala-
ika wingi wa jeshi la mbinguni wakimsifu
Mungu na kusema: "Atukuzwe Mungu juu
mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu
aliowaridhia." (Luka 2:14)

Baada ya malaika kuondoka, wachunga-
ji walianza kuzungumza wao kwa wao. "Haya,
na twendeni mpaka Bethlehemu, tukalione
hilo lililofanyika."

Wachungaji hawakujali kondoo zao.
Habari hii njema ilikuwa muhimu zaidi
kwao kuliko kitu cho chote ambacho wange-
weza kufikiria. Walikuwa wamekwisha kungo-
jea miaka mingi sana Mwokozi kuja. Kwa
hiyo hakukuwa na kitu cho chote sasa

kilichokuwa muhimu kama habari hiyo njema.

Walijiharakisha kwenda Bethlehemu, wakampata Mariamu na Yusufu na mtoto Yesu amelala horini. Walimwambia kila mtu waliyekutana naye mambo ambayo malaika waliwaambia, na kwamba walikwenda zizini kumwabudu Kristo. Walirudi makondeni huku wakimtukuza Mungu kwa mambo yote waliyosikia na kuyaona.



Zilipotimia siku nane tangu mtoto kuzaliwa, Mariamu na Yusufu walimwita jina lake Yesu kama walivyoambiwa na Mungu. Na zilipotimia siku arobaini, walimpeleka Yesu hekaluni Yerusalemu kwa sababu kila mtoto mwanamume aliye kifungua mimba katika kila jamaa ya Kiyahudi alipelekwa hekaluni na kutolewa sadaka kwa Mungu.

Kulikuwa na mtu mmoja mzee sana aliyetaka zaidi mno kumwona Mwokozi kwa macho yake mwenyewe. Mzee huyu aliitwa Simeoni. Siku moja, Simeoni alijua ya kwamba Mungu alimtaka kwenda hekaluni. Basi, wakati Mariamu na Yusufu na mtoto wao walipoingia hekaluni, yeye alikuwamo ndani akingojea. Alimwona Yesu, akampokea mikononi mwake. Alijua kwamba mtoto huyu ni Mwokozi. Wakati alipokuwa akimpokea mtoto Yesu mikononi mwake, alimshukuru Mungu kwa kujibu maombi yake. Alisema, "Sasa, Bwana, wamruhusu mtumishi wako, kwa amani, kama ulivyosema; kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu wako, uliouweka tayari machoni pa watu wote; nuru ya kuwa mwangaza wa Mataifa, na kuwa utukufu wa watu wako Israeli." Unaweza kusoma maneno hayo katika Luka 2:29-32.

Wakati Mariamu na Yusufu walipokuwa wakistaajabia maneno hayo ya Simeoni aliyemtambua mtoto wao, mwanamke mmoja mzee nabii, ambaye aliitwa Ana, alikuja kutoka mahali pa kimya mle hekaluni ambapo alikaa na kuabudu na kuomba. Yeye pia alipomwona mtoto Yesu, alimfahamu, akamshukuru Mungu kwa sababu sasa Mwanawe alikuja kukaa duniani.

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

Mungu alifanya maagano mengi katika miaka mingi na akatimiza ahadi hizo zote. Maagano hayo yalikuwa makuu, lakini agano hili la sasa (yaani, Mwanawe) lilikuwa kuu zaidi kuliko zote. Alimtoa Mwanawe pekee ili wewe na mimi tungeweza kusamehewa dhambi zetu.

Jambo la huzuni ni kwamba watu wengi hata hawana shukrani kwa Mungu kwa mambo ambayo amekwisha kuwafanyia. Wengi hawajampokea Mwana wa Mungu kama Mwokozi wao. Wanaishi kwa ajili yao wenyewe. Je! wewe umekwisha kumpokea Yesu kama Mwokozi wako? Ikiwa umekwisha kumpokea, basi una-weza kujua kwamba yeye ni Mfalme wa Amani kwa sababu umekwisha kusamehewa dhambi zako.

KAZI YA KUFANYA:

Mungu alitoa ahadi yake kwa Hawa ambaye hakuwa na furaha katika Bustani ya Edeni. Mungu alisema siku moja Mtoto wa ajabu angezaliwa. Mtoto huyo angekuwa Mwana hasa wa Mungu ambaye angeangamiza nguvu za Shetani. Wakati Mwana wa Mungu alipozaliwa, Mungu alitangaza habari ya kuzaliwa kwake kwa njia maalum.

Je! ni watu gani waliokuwa wakilinda kondoo zao usiku? _____

Je! ni nani aliyewatokea kwa ghafula? _____

Je! ni nini kilichowang'aria pande zote? _____

Wachungaji waliogopa. Je! alisema jambo gani la kuwatia moyo? _____

Je! ni nani aliyezaliwa? _____

Je! alizaliwa katika mji upi?

Mtoto huyo alilazwa ndani ya nini?

Sasa andika maneno yaliyosemwa na wingi wa jeshi la mbinguni wakati walipojiunga na malaika yule wa kwanza. Unaweza kupata maneno katika Luka 2:13-14.

Tazama katika vifungu 15-16 mambo ambayo wachungaji walifanya baada ya kusikia ujumbe wa Mungu. Kata maneno yote yaliyo katika alama hii () ambayo si kweli.

Wakati malaika waliporudi mbinguni, wachungaji waliambiana wao kwa wao, "Haya, na twendeni mpaka (Nazareti) (Bethlehemu), tukamwone mtoto huyo ambaye malaika amesema ni Kristo Bwana."

Wachungaji walikwenda (pole pole) (kwa haraka).

Waliwakuta Mariamu na Yusufu, na mtoto Yesu.

Kulikuwa na watu wachache ambao bado walimpenda Mungu na kumtii. Walisoma Maandiko ya Agano la Kale, wakatazamia wakati ambapo Mkombozi wa ulimwengu angezaliwa. Soma jinsi watu mbalimbali waliivyowaza juu ya kuzaliwa kwa Mwana wa Mungu. Kata kwa mstari maneno yote ya uwongo.

Watu walistaajabia habari za wachungaji.

Mariamu aliyaweka hayo yote moyoni mwake.

Mfalme alifurahi kwa sababu Yesu alizaliwa.

Mwenye nyumba ya wageni alijidai ya kwamba Yesu alizaliwa katika zizi lake.

Wachungaji walimtukuza Mungu na kumsifu.

Simeoni alifurahi, kwa hiyo alimsifu Mungu.

Ana pia alimsifu Mungu kwa ajili ya mtoto Yesu.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo." 2 Wakorintho 9:15

KIPAWA KIKUU CHA MUNGU

Ikiwa umekwisha kupokea kipawa cha Kristo, Je! utamshukuru?

Ikiwa umekwisha kupokea kipawa cha Mungu kwako ambacho ni Kristo, utamshukuruje? _____

Ikiwa hujampokea Yesu, Je! utampokea leo? Unaweza kuanza kuishi maisha mema kwa ajili yake na kufanya hivyo kutamwonyesha kwamba unamshukuru kwa kipawa chake kikuu kwako.

MANENO YA KUJIFUNZA:

zizi.....ua, banda, kifalu, n.k.,
cha kuwekea mifugo.

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Luka 2:8-20, 29-33, 36-39

Na katika nchi ile ile walikuwako wachungaji wakikaa makondeni na kulinda kundi lao kwa zamu usiku. (9) Malaika wa Bwana akawatokea ghafula, utukufu wa Bwana ukawang'aria pande zote, wakaingiwa na hofu kuu. (10) Malaika akawaambia, Msiogope; kwa kuwa mimi ninawalettea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; (11) maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana. (12) Na hii ndiyo ishara kwenu; mtamkuta mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto, amelala katika hori ya kulia ng'ombe. (13) Mara walikuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

la mbinguni, wakimsifu Mungu, na kusema,

(14) Atukuzwe Mungu juu mbinguni,

Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia. (15) Ikawa, malaika hao walipoondoka kwenda zao mbinguni, wale wachungaji waliambiana, Haya, na twende-ni mpaka Bethlehemu, tukalionge hilo lili-
lofanyika, alilotujulisha Bwana. (16) Wakaenda kwa haraka wakamkuta Mariamu na Yusufu, na yule mtoto mchanga amelala horini. (17) Walipomwona wakatoa habari waliyoambiwa juu ya huyo mtoto. (18) Wote waliosikia wakastaajabu kwa hayo waliyoambiwa na wachungaji. (19) Lakini Mariamu akayaweka maneno hayo yote, akiyafikiri moyoni mwake. (20) Wale wachungaji wakarudi, huku wanamtukuza Mungu na kumsifu kwa mambo yote waliyosikia na kuyaona, kama walivyoambiwa.

2:29-33

Sasa, Bwana, wamruhusu mtumishi wako, Kwa amani, kama ulivyosema; (30) Kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu wako, (31) Uliouweka tayari machoni pa watu wote; (32) Nuru ya kuwa mwangaza wa Mataifa, Na kuwa utukufu wa watu wako Israeli. (33) Na babaye na mamaye walikuwa wakiyastaajabia hayo yaliyonenwa juu yake.

2:36-39

Palikuwa na nabii mke, jina lake Ana, binti Fanueli, wa kabila ya Asheri, na umri wake ulikuwa miaka mingi, alikuwa amekaa na mume miaka saba baada ya uanawali wake. (37) Naye ni mjane wa miaka themanini na minne; haondoki katika hekalu, ila huabudu usiku na mchana kwa

kufunga na kuomba. (38) Huyu alitokea
saa ile ile akamshukuru Mungu, na wote
waliokuwa wakiutarajia ukombozi katika
Yerusalemu akawatolea habari zake. (39)
Basi, walipokwisha kuyatimiza yote kama
yalivyoagizwa katika sheria ya Bwana,
walirejea Galilaya mpaka mjini kwao,
Nazareti.

MPANGO HALISI WA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Mwanzo 2:16-17;
Mwanzo 3:1-6; Isaya 53:6; Warumi
1:18; 6:23; Waebrania 9:12; Waefeso
1:7

Mungu aliumba ulimwengu mzuri. Wakati kila mojawapo ya vitu ambavyo Mungu aliumba kilipokuwa tayari, Mungu aliumba kitu kingine. Mungu hakuumba maua mpaka alipoumba ardhi, mwangaza wa jua, na maji kwanza kwa ajili yao. Hakuwaumba wanyama mpaka alipowaumbia mimea ya kula. Hakumwumba mwanadamu mpaka alipokwisha kuumba vitu vingine vyote kuwa tayari. Mungu aliumba vitu vyote vizuri kwa ajili ya mwanadamu kuvifurahia. Alimwumba mwanadamu ili angeweza kuwa urafiki mwema naye na kushiriki naye pamoja. Mungu alimkusudia mwanadamu kufurahia vitu vyote alivyoumba. Alimpa mwanadamu usimamizi juu ya vitu vyote.

Kulikuwa na amri moja pekee ambayo Mungu alimpa mwanamume na mwanamke wa kwanza. Je! unakumbuka amri hiyo? Aliwaambia wasile tunda la mti mmoja, Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya. Lakini mwanamume na mwanamke wale walichagua kutomtii Mungu. Walifikiria tamaa zao wenyewe za choyo, wakala matunda ya mti ule waliokatazwa. Hivyo dhambi iliingia ulimwenguni kuvunja ushirika ambao Mungu alipanga kati yake ya mwanadamu. Watu hawa wawili hawakutenda dhambi peke yao, bali kila mmoja ulimwenguni ametenda dhambi isipokuwa Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Yeye

peke yake ndiye hakuwa na dhambi hata kidogo.

Mungu hakuacha kumpenda Adamu na mkewe ingawa walichagua kutomtii. Aliwahidi kitu ambacho hawakustahili. Aliwahidi Mwokozi ambaye angelipia deni la dhambi waliyofanya. Je! ni nani ambaye angefanya hivyo? Ndiyo, Mungu alipanga kutuma Mwanawe kupipa deni la dhambi ya kila mtu. Huu ulikuwa mpango wa ajabu wa Mungu alipanga kuwaokoa watu wake. Angewalipia deni lao ili kuwaokoa katika utumwa wa dhambi zao.

Tangu zamani Mungu aliwaambia watu jambo la kufanya ili waweze kuokolewa. Habili alimtii Mungu akamtolea sadaka katika njia ambayo Mungu aliwaambia kufuata. Mungu alipendezwa na sadaka yake kwa sababu alifanya kama Mungu alivyosema. Lakini Kaini hakufuata mafundisho ya Mungu na Mungu hakupendezwa na sadaka yake. Je! unakumbuka hadithi juu ya ndugu hawa wawili? Ilikuwa muhimu kumwaga damu ili dhambi ingeweza kusamehewa. Habili alikuwa mchungaji, kwa hiyo alitoa sadaka ya mnyama. Lakini Kaini alikuwa mkulima, na alitoa sadaka ya mazao yake ya ardhi. Sadaka hii haikuhusu umwagaji damu, kwa hiyo ilikuwa ni kutoamtii Mungu. Dhambi hii ya kutotii ndiyo iliyokuwa moja kati ya dhambi nyingi maishani mwa Kaini. Kwa sababu ya dhambi hii, Mungu alimwadhibu.

Siku moja, Mungu alimwita Abram kuwa kichwa cha taifa maalum. Mungu aliagana naye. Alisema taifa la Abram

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

lingekuwa baraka kwa ulimwengu wote. Waebrania 9:12 inatuonyesha kwamba Mwokozi wa ulimwengu alizaliwa katika taifa la Abram. Yeye ni Bwana wetu Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.

Haukuwa mpango wa Mungu mwanadamu kukaa katika dhambi na huzuni, lakini mwanadamu alipochagua kitu tamaa zake mwenyewe za uchoyo badala ya kumtii Mungu, Mungu alifanya mpango. Mpango huu ulikuwa wa thamani kubwa kwa Mungu kwa sababu ulihitaji Mwanawe pekee, Yesu Kristo. Hakukuwa na mtu mwingine ambaye angeweza kulipa deni la dhambi kwa sababu kila mtu alikuwa mwenye dhambi. Hakuna mtu ambaye angeweza kujiokoa mwenyewe, lakini Yesu hakuwa na dhambi, kwa hiyo yeye peke yake ndiye angeweza kulipa deni la dhambi.

Mungu aliahidi kumtuma Mwanawe siku moja ulimwenguni. Aliwaambia watu wengi habari kuhusu mpango huu wake. Tunaweza katika Agano la Kale habari kuhusu ahadi hii tangu mwanzo mpaka wakati ambapo Yesu alikuja. Manabii walihubiri ahadi hii ya Mungu. Alitaka watu wake kujua kwamba angewaokoa.

Wakati aliopanga Mungu ulipofika, Yesu alizaliwa zizini Bethlehemu akalazwa katika hori ya kulia ng'ombe. Wakati huu ahadi zote za Mungu zilitimilika. Yesu ndiye aliyekuwa kila jambo na kila ahadi ambayo Mungu aliahidi.



Mungu alitwambia juu ya mpango wake katika kitabu chake ambacho ni Biblia. Mpango huo wake ni rahisi sana hata mtoto mdogo anaweza kuuelewa na kupokea kipawa cha Mungu cha wokovu. Kama tukiwa na imani katika Yesu Kristo, atatuokoa

katika dhambi zetu.

KAZI YA KUFANYA:

Rudia maelezo ya Biblia jinsi dhambi ilivyoingia ulimwenguni. Andika herufi "X" kwenye mistari iliyo kando ya maneno ya kweli.

- Mungu aliwapa mume na mke wa kwanza mahali pazuri sana pa kukaa.
- Mungu alimpa Adamu amri nyingi ngumu kuzitii.
- Mume na mke wa kwanza walichagua kutomtii Mungu.
- Mume na mke wa kwanza walitenda dhambi kwa kufanya mambo waliyoambiwa na Shetani.

Sasa soma jinsi dhambi ilivyoenea kwa kila mtu. Andika herufi "X" kwenye mstari ulio kando ya sentensi ya kweli. (Soma Isaya 53:6)

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

___ Tumechagua kufuata n'ia ya Mungu.

___ Bwana Yesu Kristo amechukua dhambi yetu sisi sote katika mwili wake.

Mungu hakuacha kuwapenda watu alio-
waumba ingawa walikuwa wametenda dhambi.
Mungu alifanya mpango wa ajabu. Angewali-
pia watu deni la dhambi zao ili kuwafanya
kuwa huru kutokana na utumwa wa dhambi
hizo. Je! ni kitu gani kilichokuwa muhimu
kuleta msamaha wa dhambi?

Katika siku za Agano la Kale, watu
walimtii Mungu na walimtolea sadaka ya
wanyama madhabahuni kuonyesha kwamba
walisikitika kwa ajili ya dhambi yao.
Siku hizi hatutoi sadaka ya wanyama. Je!
ni kwa nini? (Soma Waebrania 9:12)



Sasa soma Vifungu vingine juu ya mpango wa Mungu wa kutuokoa katika dhambi yetu. Kata maneno yote yaliyo katika alama hii () ambayo si kweli.

Mungu ni mtakatifu. Huonyesha (hasira) (ufahamu) yeye juu ya udhalimu au juu ya dhambi. Matokeo ya (ugonjwa) (dhambi) ni mauti ya milele. Lakini kipa-wa cha bure cha Mungu ni uzima wa milele katika Kristo ambaye ni Mwokozi.

Soma tena Waebrania 9:12 na Waefeso 1:7. Sasa andika kwa maneno yako mwenyewe mpango wa Mungu wa wokovu.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Na ya kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu."

2 Timotheo 3:15

Biblia ni kitabu cha ajabu mno! Mpa-ngo wa Mungu wa wokovu ni rahisi sana hata mtoto mdogo anaweza kuuelewa na kuo-kolewa. Soma tena kifungu hicho cha kuku- mbuka, kisha chora mviringo kwa jibu la kweli.

Unawezaje kuhekimishwa hata upate wokovu?

Kwa kuwa mwema

Kwa imani tha-
biti.

Kwa kulipa pesa

Kwa kuwaiga
wazazi wangu

Je! unapaswa kuweka imani yako
katika nani?

Mchungaji wangu

Mimi mwenyewe

Wazazi wangu

Yesu Kristo,
Mwana wa Mungu

Je! umehekimishwa hata kupata woko-
vu? Je! umekwisha kumwomba Yesu kuwa
Mwokozi wako?

MANENO YA KUJIFUNZA:

VIFUNGU VYA BIBLIA:

Mwanzo 2:16-17

BWANA Mungu akamwagiza huyo mtu,
akisema, Matunda ya kila mti wa bustani
waweza kula, (17) walakini matunda ya
mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa
maana siku utakapokula matunda ya mti huo
utakufa hakika.

MPANGO HALISI WA MUNGU

Isaya 53:6

Sisi sote kama kondoo tumepotea;
Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwe-
nyewe; Na BWANA ameweka juu yake Maovu
yetu sisi sote.

Waebrania 9:12

wala si kwa damu ya mbuzi na ndama,
bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara
moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata
ukombozi wa milele.

Mwanzo 3:1-6

Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko
wanyama wote wa mwitu aliowafanya BWANA
Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! hivi
ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda
ya miti yote ya bustani? (2) Mwanamke
akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya
bustani twaweza kula; (3) lakini matunda
ya mti ulio katikati ya bustani Mungu
amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije
mkafa. (4) Nyoka akamwambia mwanamke,
Hakika hamtakufa (5) kwa maana Mungu
anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda
ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi
mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.
(6) Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti
wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao
ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi
alitwaã katika matunda yake akala, akampa
na mumewe, naye akala.

Warumi 1:18

Kwa maana ghadhabu ya Mungu imedhi-
hirishwa kutoka mbinguni juu ya uasi wote
na uovu wa wanadamu waipingao kweli kwa
uovu.

KUANZIA ADAMU MPAKA IBRAHIMU

Warumi 6:23

Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.

Waefeso 1:7

Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake.